

# NYIMBO ZA WANATAI

## TABLE OF CONTENT

TABLE OF CONTENT .....	i
1. NURU YA JIONI .....	1
2. LILE JIWE JEUPE .....	1
3. UNYAKUZI.....	1
4. HUYU NDIYE BIBI-ARUSI.....	2
5. BI-ARUSI WA OMEGA ALIYEREJESHA.....	2
6. USINIPITE MKOMBOZI WANGU NATAMANI UKAMILIFU .....	2
7. NI WAKATI WA KUTENGANA .....	3
8. HII NDIYO EFESO .....	3
9. MTO WA NENO TIMILIFU .....	4
10. UTEUZI WA MUNGU .....	4
11. BADILISHA JINA LANGU KUPITIA UFUNUO. ....	4
12. UFUNUO WA MBEGU CHINI YA MUHURI WA SABA.....	5
13. ABUDU MWANA-KONDOO MKOMBOZI .....	5
14. MAHALI TEULE PA IBADA YA KRISTO YESU .....	5
15. SAUTI YA MALAIKA MKUU NDANI YANGU.....	6
16. DEEPER DEEPER.....	6
17. FATHER LET THE FIRE FALL.....	7
18. COME BY HERE .....	7
19. MINE MINE MINE .....	7
20. FIRE FIRE FIRE .....	7
21. WHAT A MIGHTY GOD .....	7
22. LEARNING TO LEAN .....	7
23. THIS IS THE DAY.....	7
24. HALLELUYAH .....	7
25. IN THE NAME OF JESUS.....	8
26. I'M GLAD JESUS SET ME FREE .....	8
27. THE ORIGINAL LIFE .....	8
28. WE ARE MARCHING OVER .....	8
29. SEE YOU IN THE RAPTURE .....	8
30. BY HIS WORD .....	8
31. BI-ARUSI AMEBARIKIWA NA BARAKA ZOTE ZA KIROHO .....	9
32. MAJINA SABA YA UKOMBOZI.....	9
33. MATENDO YAKO .....	10



34. NATAMANI KURUDI NYUMBANI .....	10
35. TUASHENI TAA ZETU .....	10
36. BI-ARUSI AMEZUKIWA NA JUA LA HAKI .....	11
37. UBATIZO WA MAJI KWA JINA LA BWANA YESU KRISTO WAKATI HUU.....	11
38. JINA LANGU LAITWA CHINI YA MUHURI WA SABA.....	12
39. KUTEMBEA NA ELOHIMU NIKAMILIKE.....	12
40. UKOMBOZI WETU WADHIHIRISHA UTUKUFU WA MUNGU .....	12
41. UKINGONI MWA YORDANI .....	13
42. UNYAKUZI WA BI-ARUSI KWENDA KARAMUNI.....	13
43. GOD WILL MAKE A WAY.....	13
44. CAN'T YOU SEE WHY I AM SO HAPPY .....	13
45. JESUS IS THE WINNER MAN .....	13
46. ELIEZER'S CAMEL TRAIN .....	14
47. HUKUMU BAADA YA KARAMU NA MIAKA ELFU .....	14
48. MEZA YA BWANA .....	14
49. MIMI NI MSAFIRI.....	15
50. KUTAWADHANA MIGUU .....	15
51. ROHO ATANGAZA HAKUNA WAKATI TENA.....	15
52. KUWEKWA WAKFU WATOTO .....	15
53. WIMBO WA KUWAIMBIA WALIOPOSANA .....	16
54. MWILI WANGU WA NENO WANIITA.....	16
55. KUPAA KWA TAI KATIKA AHADI ZA WAKATI .....	16
56. KUJA KWA BWANA KU NDANI YA BI-ARUSI WA KIZAZI. ....	17
57. WAKATI UNAISHA. ....	17
58. NI WAKATI WA KWENDA NYUMBANI.....	17
59. IBADA YA MWANAKONDOO WA MUNGU.....	18
60. YESU KRISTO MSAMARIA MWEMA.....	18
61. A) NI TAMU KUMJUA YESU .....	18
61. B) TIS SO SWEET TO TRUST IN JESUS .....	18
62. UNIUMEGEE MKATE HAI.....	19
63. NINATUMAINI YESU MKOMBOZI WANGU.....	19
64. HAPO KATIKA ENEO LA SABA .....	19
65. IT'S ALL OVER ME .....	19
66. UFALME WA JIWE .....	20
67. BI-ARUSI AMEKARIBIA KWENDA.....	20
68. BWANA HEBU NIWEPO BI-ARUSI AIGIAPU .....	20
69. UKOMBOZI MKAMILIFU .....	20



70. IN HEAVEN I WILL.....	21
71. CHA KUTUMAINI SINA.....	21
72. JESUS TOOK MY BURDENS.....	21
73. JESUS IS MINE.....	21
74. SERVING THE LIVING GOD.....	21
75. NAKUPENDA BWANA YESU.....	21
76. A) FURAHA KUU ANGANI .....	22
76. B) GREAT JOY IN THE AIR .....	22
77. OH LORD, HERE I AM, RIPEN ME.....	22
78. A) NARUDI NYUMBANI BWANA.....	22
78. B) LORD I AM COMING HOME .....	22
79. A MYSTERIOUS CLOUD.....	23
80. NEVER GET WEARY YET.....	23
81. YUBILE YA WAKATI WA MWISHO .....	23
82. MUNGU AKINENA KUPITIA BI-ARUSI .....	23
83. MARA NYINGINE BWANA.....	24
84. MUNGU WANGU BABA UMENITOSHA .....	24
85. MAOMBI YANGU BWANA .....	24
86. LORD JESUS YOU DESERVE THE GLORY.....	24
87. HOW DEEP THE FATHER’S LOVE .....	24
88. I’VE GOT TO PROVE I’M ONE IN A MILLION .....	25
89. WE COME FROM FAR.....	25
90. HIS NAME IS JESUS CHRIST.....	25
91. UKOMBOZI NA UHAMISHO .....	25
92. KUJITAMBUA NA KWENDA UNYAKUZI.....	26
93. BI-ARUSI KATIKA CHUMBA CHA KUVAA.....	26
94. WIMBO WA HARUSI.....	26
95. YEHOVAH WA AGANO LA KALE NDIYE YESU WA JIPYA .....	27
96. AGANO JIPYA.....	27
97. NJIWA NA TAI.....	27
98. A) BWANA UMEBADILISHA USHUHUDA WANGU.....	28
98. B) LORD YOU’VE CHANGED MY TESTIMONY .....	28
99. A) KUVUKA YORDANI HADI KANANI SIKU YA LEO.....	28
99. B) CROSSING OVER JORDAN TO CANAAN LAND THIS DAY .....	29
100. SIRI YA MUHURI WA SABA .....	29
101. WINGU LA KIUNGU ISHARA YA MWISHO .....	29
102. THE RAPTURE TRAIL OF THE BRIDE.....	30



103. YESU MJI WA MAKIMBILIO .....	30
104. ASANTE KWA KUNIFUNULIA UNYAKUZI .....	30
105. A) KUHUIHWA KWA UWEZO WA BI-ARUSI .....	30
105. B) QUICKENING OF THE POTENTIALS OF THE BRIDE .....	31
106. MALAIKA WA AGANO KATIKA KUTOKA .....	31
107. A) ITWAE NAFASI YAKO EWE BI-ARUSI .....	31
107. B) STEP INTO YOUR POSITION BRIDE .....	32
108. KANISA LA KILELE LILILOAHIDIWA.....	32
109. A) NAKUABUDU MUNGU BABA .....	32
109. B) I WORSHIP YOU FATHER GOD .....	32
110. A) MAISHA YA TAI .....	33
110. B) EAGLE LIFE .....	33
111. KUREJESHA KWA KANISA LA MITUME.....	33
112. BWANA AMWENDESHA FARASI TENA KATIKA BI-ARUSI .....	33
113. A) KUFUNULIWA KWA MWANA WA ADAMU.....	34
113. B) THE REVELATION OF THE SON OF MAN .....	34
114. A) KUTOKA KWA TATU .....	35
114. B) THE THIRD EXODUS.....	35
115. A) BWANA YESU KRISTO NI EBENEZERI.....	35
115. B) LORD JESUS CHRIST IS EBENEZER .....	35
116. A) MAISHA YA AYUBU KIVULI CHA UKOMBOZI.....	36
116. B) JOB'S LIFE TYPING REDEMPTION .....	36
117. A) NDUGU YANGU MKUBWA ALIBEBA MZIGO WANGU .....	36
117. B) MY BIG BROTHER BORE MY BURDEN .....	37
118. A) USHIRIKA NAWA YESU NDIO SHAUKU YANGU .....	37
118. B) YOUR FELLOWSHIP JESUS IS MY DESIRE.....	37
119. A) SAA YA ILE ISHARA.....	37
119. B) THE HOUR OF THE TOKEN .....	38
120. A) MWANA-KONDOO KWA AJILI YA KUTOKA.....	38
120. B) THE LAMB FOR EXODUS .....	38
121. A) YUSUFU MFANO WA KRISTO NA BI-ARUSI.....	39
121. B) JOSEPH A TYPE OF CHRIST AND BRIDE .....	39
122. A) KUREJESHA KWA KANISA LA KIMITUME .....	39
122. B) RESTORATION OF THE APOSTOLIC CHURCH .....	40
123. A) JIBU LA BI-ARUSI KWA MWOVU SHETANI.....	40
123. B) THE BRIDE'S ANSWER TO THE DEVIL .....	40
124. A) KUJENGA TENA HEKALU HAI WAKATI HUU .....	41



124. B) REBUILDING OF THE LIVING TEMPLE IN THIS TIME .....	41
125. A) UREJESHO NA KUKOMAA KWA BI-ARUSI .....	41
125. B) RESTORATION AND MATURITY OF THE BRIDE .....	42
126. A) WEKA ISHARA KWA JAMAA YAKO .....	42
126. B) APPLY THE TOKEN TO YOUR FAMILY .....	42
127. A) KUAMKA KWA ESTA.....	43
127. B) AWAKENING OF ESTHER.....	43
128. A) MWANAMKE MSHUNAMI MFANO WA KANISA LA ALFA NA OMEGA .....	43
128. B) THE SHUNAMITE WOMAN A TYPE OF ALPHA AND OMEGA CHURCH.....	44
129. A) UDHIRISHO WA MBEGU ZA KIROHO ZA MUNGU .....	44
129. B) THE EXPRESSION OF GOD'S SPIRITUAL GENES .....	44
130. A) BI-ARUSI APELELEZA AHADI YA WAKATI.....	45
130. B) THE BRIDE SEEKING THE PROMISE OF THE HOUR.....	45
131. A) KUTOKA LAODIKIA HADI IMANI YA UNYAKUO .....	45
131. B) FROM LAODICEA TO RAPTURING FAITH.....	46
132. A) BI-ARUSI AKIWA NA VAZI LA ELIYA NA NGUVU ZA MUNGU .....	46
132. B) THE BRIDE WITH THE ROBE OF ELIJAH AND POWER OF GOD.....	46
133. A) WIMBO WA SHEREHE YA HARUSI .....	47
133. B) WEDDING CEREMONY SONG.....	47
134. A) HAZINA YA BETHLEHEMU .....	47
134. B) BETHLEHEM'S TREASURE.....	48
135. A) AMANI KWAKO BI-ARUSI.....	48
135. B) SHALOM UNTO YOU BRIDE.....	48
136. A) MIKAYA SHAHIDI WA KWELI.....	49
136. B) MICAH A TRUE WITNESS .....	49
137. A) KUFA NA KUFUFUKA KWA LAZARO VYAFUNUA UKOMBOZI.....	49
137. B) LAZARUS DEATH AND RESURRECTION REVEAL REDEMPTION .....	50
138. A) USIOGOPE BI-ARUSI MDOGO .....	50
138. B) FEAR NOT LITTLE BRIDE .....	50
139. A) BI-ARUSI AFANYIKA UNABII WAKE .....	51
139. B) THE BRIDE BECOMING HER OWN PROPHECY .....	51



## **1. NURU YA JIONI**

1. Zacharia aliona nuru ya neno  
Imekuja wakati wa jioni  
Yehova akiwa Mfalme duniani  
(Akiwa Bwana aliye na jina moja) x2

**Ni siku moja Bwana aijua,  
Kuna nuru na tena kuna giza,  
Lakini jioni ifikapo  
(Nuru inaangazia nafsi yangu) x2**

2. Ibrahimu alituma Elieza  
Amletee Isaka Bi-arusi  
Ilikuwa wakati wa jioni,  
(Kampata Rebeka tena kampeleka) x2
3. Mungu kamtuma Musa anenee Israeli  
Jioni wachinje mwana kondoo  
Damu nayo wapake milangoni  
(Kusiwe kifo kama kwa Wamisiri) x2
4. Eliya na manabii hao wa Baali,  
Wakakutana wakati wa jioni,  
Ijulikane Mungu gani wa kweli,  
(Utukufu wa Yehova ukaenea) x2
5. Wanafunzi Cleopasi na rafikiye,  
Wakakutana na Yesu jioni,  
Kawafunulia unabii wa neno,  
(Alipomega mkate wakamjua) x2
6. Malaika hao saba wakamjia,  
Nabii mlimani huo wa machweo  
Akatumwa aende akahubiri,  
(Siri hiyo ya mihuri saba) x2
7. Nuru ya jioni ndani ya Bi-arusi,  
Amjua Bwana amegewa mkate,  
Akiwa Mfalme na tena akiwa Bwana,  
(Aliye na jina moja la ukombozi) x2
8. Umeipokea nuru ya jioni?  
Ndio Imani ya mababa zetu?  
Na tena Imani hii ya unyakuzi?  
(Tuite waliolala twende nyumbani) x2

## **2. LILE JIWE JEUPE**

1. Huyu ni nani anashuka wingu amejivika?  
Kitabu amefungua ni Malaika mkuu,  
Uso wake kama jua miguu ni nguzo za moto,  
Upinde kichwani mwake anao ujumbe gani?

**(Tulia hapo rafiki tazama jiwe jeupe  
Jua halijawahi angazia jiwe hili) x2**

2. Malaika amekanyaga bahari na nchi kavu,  
Sauti kuu akatoa kama simba angurumaye,  
Sauti zikatolewa na hizo ngurumo saba,  
Bi-arusi analishwa na ufunuo wa jiwe.
3. Junior Jackson akaona jiwe jeupe ndotoni  
Nabii alipofunua mlima juu na mtaimbo,  
Nabii akawaelezea watazame jiwe hilo,  
Wachache waliobaki ndio Bi-arusi wa Yesu.
4. Huyu nabii alihubiri siri za mihuri saba,  
Huo muhuri wa saba ulikuwa wa ajabu,  
Ulikuwa umenyamaza uhai ukipanwa,  
Hili jiwe jeupe ndilo unyakuzi wangu.
5. Baada ya kupokea jiwe hili jeupe,  
Bi-arusi anapokea jina jipya la Yesu,  
Anaanza dhahirisha maisha ya Yesu Kristo,  
Halleluya, Halleluya Yesu nipe jiwe hili.
6. Danieli alitazamia, pia manabii wengine,  
Wapokee hili jiwe ndani ya nafsi zao,  
Lakini ukweli ni kwamba jiwe hili ni langu,  
Sasa ninashangilia jiwe hili ni langu.

## **3. UNYAKUZI**

1. Paulo alionyeshwa Yeye akirudi,  
Bwana-arusi akiitana kwa mwaliko,  
Ndio ujumbe huo wa Malaki nne,  
Ufunuo kumi unyakuzi wangu.

**Hili ni njambo limekuwa sirini,  
Ya kwamba mimi sitaonja mauti,  
Nitaishi hadi Yesu arudi,  
(Mwili ubadilishwe tukutane angani) x2**

2. Ni dhahiri kwamba tutanyakuliwa,  
Kwani Elija na Enoko walipaa,  
Baada ya kuishia neno la Mungu,  
Wakashinda vita na kwenda nyumbani.
3. Yesu anarudi achukue neno lake,  
Ujavu wake na tena mpenzi wake,  
Namtamani na yeye anitamani,  
Mpenzi wangu tuishi naye milele.
4. Baada ya Yesu Kristo kufufuka,  
Watakatifu wa kale wakafufuka,  
Wakaonekana na wanafunzi wa Yesu,  
Wakanyakuliwa huko ng'ambo ya pazia.



5. Bi-arusi ana nguvu za uumbaji,  
Tuite watakatifu wafufuke,  
Tukae nao kwa muda mfupi,  
Tubadilishwe tunyakuliwe pamoja.
6. Baada ya miili yetu kubadilishwa,  
Adui shetani hatatuona tena,  
Nguvu za kifo na kaburi ziishe,  
Mshale wako shetani uko wapi?
7. Tukikutana na Yesu kule angani,  
Nitafurahi hata nimkumbatie,  
Nimwabudu na tena nimuinue,  
Mpenzi wangu kweli wa ajabu.

#### **4. HUYU NDIYE BIBI-ARUSI**

1. Bwana-arusi anonokea kiti,  
Cha uombezi na sasa ameshuka,  
Kuja kudai kile alichofia,  
Ndugu na dada hebu kwanza jihoji.

**Ni ufunuo wa Yesu ni ufunuo,  
Ni ufunuo wa Bibi Arusi,  
Warejesha Bi-Arusi nyumbani,  
Ili turudi kule tulipotoka.**

2. Vikundi na watu wanadai,  
Wakisema hao ni Bibi-arusi,  
Lakini neno litasimama,  
Ni ufunuo wa zile ngurumo saba.
3. Washangaa Bi-arusi ni nani,  
Bi-arusi amejivika neno,  
Amejazwa na Roho mtakatifu,  
Adhihirisha neno la Bwana-arusi
4. Nabii alihubiri neno,  
Akaonyesha Bi-arusi ni nani,  
Amejivika koti la yule Yusufu,  
Adhihirisha ukamilifu wa Neno.
5. Walia wewe huna mguu,  
Walia wewe huna mkono,  
Bi-arusi tayari amejitambua,  
Shida zote zinapata suluhu.
6. Wahitaji neno la kunyakuliwa,  
Wahitaji neno la kunena,  
Kimbilia Ngurumo saba sasa,  
Dhiki kuu imo hapo mlangoni.

#### **5. BI-ARUSI WA OMEGA ALIYEREJESHA**

1. Hii ni ahadi ya siku za mwisho,  
Imani ya mitume ndio Baba zetu,  
Itarejeshwa Kanisani mwa Mungu,  
Ajidhihirishe tena duniani.

**Amerejeshwa Bi-arusi wa Omega,  
Amerejeshwa na mwaliko wa Bwana Yesu,  
Na utukufu mwingi kuliko wa kwanza,  
Nimerejeshwa mimi nimerejeshwa.**

2. Alipowaumba, Hawa alijaribiwa,  
Na kuvunja neno walilopewa,  
Adamu na Hawa wa mwisho wamerejeshwa,  
Kwa utawala miaka elfu moja.
3. Samsoni alijawa na nguvu za Mungu,  
Akapana siri akanyolewa nywele,  
Adui wakaja na kumng'oa macho  
Nguvu ikarejeshwa akafanya maajabu.
4. Israeli walipotoka nyumbani,  
Na kwenda nchini ya ugeni,  
Shida na dhiki nyingi ziliwafuata  
Kirudi nyumbani wanabarikiwa.
5. Kaona ono la Bi-arusi wa Alpha,  
Na utukufu mwingi, nabii akafurahi sana,  
Tena akaona kanisa la madhehebu,  
Akalia sana kwa kazi ya bure.
6. Sauti ikanena 'wacha kulia,  
Bi-arusi wa Yesu atarejea tena',  
Nabii akamuona Bi-arusi wa Omega,  
Na utukufu mwingi akamsifu Mungu.
7. Bi-arusi wa Omega yeye anarejeshwa,  
Kwa ufunuo wa muhuri wa saba,  
Kupitia huduma za vipawa tano,  
Tukamilike tudhihirishe Yesu
8. Umerejeshwa kwa ufunuo wa Yesu?  
Tai mkubwa anaitana juu,  
Nyosha mabawa na upae angani,  
Wewe ni tai twende nyumbani.

#### **6. USINIPITE MKOMBOZI WANGU NATAMANI UKAMILIFU**

1. Ibrahimu alimuona Yehova,  
Kamlilia usinipite Muumba,  
Baada ya ufunuo wa siri za Mungu,  
Miili ikageuzwa wakabarikiwa.



**Usinipite ewe Mkombozi wangu,  
Nakungojea unibariki Bwana,  
Nafsi yangu ina kiu juu yako,  
Nidhihirishe ukamilifu wako.**

2. Yakobo alipokutana na Malaika,  
Hakumpita na hakumwachilia,  
Akabarikiwa ilipofika asubuhi,  
Kwa ujasiri akakutana na Esau.
3. Batimayo kamwita Mkombozi  
Akipita ili amponye macho,  
Yesu akamwona na kumponya macho,  
Akamsifu Mungu aliye hai.
4. Alipofufuka Yesu akawaeleza,  
Wanafunzi wawili unabii wa neno,  
Wakamsihi asipite nyumbani,  
Alipomega mkate wakamjua.
5. Kama swara aliye nyikani,  
Na kiu kingi akililia maji,  
Nafsi yangu ndivyo ina kiu juu yako,  
Nidhihirishe ukamilifu wako.
6. Bi-arusi aona kiu amiliki,  
Ahadi zile amehidiwa leo,  
Apokee uhai wa Neno adhihirishe,  
Neno la kunena liwe maisha yake
7. Una kiu cha nuru ya jioni?  
Lilia Yesu asikupite sasa,  
Heri waonao njaa na kiu cha haki,  
Maana hao watashibishwa.

## **7. NI WAKATI WA KUTENGANA**

1. Dathani na Korah wakainukia Musa,  
Mungu akanena Israeli watengane,  
Wengine waende upande wa Musa,  
Dathani na wengine wakaangamia.

**(Huu) ni wakati, kweli, wa utengano,  
Kwani Bi-arusi sasa amejitambua,  
Amekuwa neno la Mungu lililo mwilini,  
Nadhihirisha huyu,  
(Bwana wangu) x2**

2. Wakatengana kwa ajili ya malisho,  
Ibrahimi kaeleza Loti achague,  
Kwenye anataka, akachagua nyikani,  
Ibrahimi akapanda mlimani.

3. Yesu alinenea wanafunzi sabini,  
Ikawa wale mwili wake, damu wanywe,  
Walibaki kumi na wawili,  
Neno la wakati likatenganisha
4. Anapoweka nyavu hiyo majini,  
Anavua viumbe aina nyingi,  
Samaki na vingine anatenganisha,  
Samaki anachukua vingine anatupa.
5. Bi-arusi anapokea ufunuo,  
Wa ngurumo saba, tukamilishwe,  
Wengine watuacha na kwenda zao,  
Kwani hata mwanzo hawakuwa wetu.
6. Twatenganishwa na unabii wa neno,  
Magugu yote yanasanywa pamoja,  
Bi-arusi anapokea ufunuo,  
Wa Bwana arusi ili twende nyumbani.

## **8. HII NDIYO EFESO**

1. Tazama pale Edeni mwana aliye dhahirishwa,  
Maumbile yatambua kwamba ni mwana wa Mungu,  
Akisema mti ung'oke uende mahali pengine,  
Hiyo sio ya ajabu maana hiyo ndiyo Efeso

**Urithi wangu wote uko ndani ya Efeso  
Efeso Kaanani yangu yenye nilihadiwa x2**

2. Yoshua yule mwana wa Nuni, alipofika Kaanani,  
Aligawa ule urithi kulingana na kabila,  
Naye shujaa Kalebu kamwambia yule Yoshua,  
"Unipe mlima wangu", maana hiyo ndiyo Efeso.
3. Baada ya matembezi ya huyu Elohimu,  
Ibrahimi na Sarah wakabadilishwa miili,  
Nabii Branham msitu wa Colorado,  
Alionjeshwa ujana, maana hiyo ndiyo Efeso.
4. Tumwache wapi Yesu baada ya ufufuo,  
Alipitia ukuta kaungana na mitume,  
Mitume wakashangaa, 'Ni jambo gani hili?'  
Lakini hawakuelewa kwamba hiyo ndiyo Efeso.
5. Efeso ndiyo nchi yetu iliyo na ahadi zetu,  
Tukitoka utumwani tupokee urithi wetu,  
Mitume walibatizwa na Roho Mtakatifu,  
Na wakazaliwa upya maana hiyo ndiyo Efeso.
6. Bi-arusi amezaliwa chini ya muhuri wa saba,  
Adhihirisha uhai wa Mumewe Elohimu,  
Atenda mambo makuu ya ajabu ya kutisha,  
Kulingana na ahadi maana hiyo ndiyo Efeso





## **9. MTO WA NENO TIMILIFU**

1. Ezekieli aliona ono la ufunuo,  
Maji yakitoka pembeni mwa nyumba,  
Akanenewa apime kina cha maji hayo,  
Kwenda chini ikawa hatua nne.  
  
**Ingia ndani ya mto uogele ndani,  
Yatiririka toka kwa Elohimu,  
Samaki wakubwa wamechangamka sana,  
Wamuinua mkombozi na kumsifu sana,  
(Kwa ajili ya ufunuo wa Mwana wa Adamu) x2**
2. Akaingia majini mara yake ya kwanza,  
Maji yakamfika vifundoni,  
Huo ni ujumbe mtumishi Luther aliohubiri,  
Wenye haki waishi kwa imani.
3. Akasongea majini hatua ya pili,  
Maji yakamfika magotini,  
Huo ni ujumbe Wesley aliohubiri,  
Maisha matakatifu yadhahirishwe,
4. Akasongea majini hatua ya tatu,  
Maji yakamfika kiunoni,  
Huo ni ujumbe pentekoste waliohubiri,  
Vipawa vya Roho vidhahirishwe.
5. Akasongea majini hatua ya nne,  
Mto wa kuogelea ukaonekana,  
Huo ni ufufuo wa zile Ngurumo saba,  
Ukombozi wote udhahirishwe.
6. Huyu nabii Branham aliohubiri,  
Ufunuo wa ile mihuri saba,  
Mto mkubwa wa uzima umedhahirishwa,  
Tunaogelea ndani ya ahadi zetu.
7. Bi-arusi aogelea mtoni huo,  
Ili tupokee ukamilifu wa neno,  
Fanya hima uogele mtoni huo,  
Maana ndio unaturudisha nyumbani.

## **10. UTEUZI WA MUNGU**

1. Ilikuwa ni vita toka tumboni mwa mama,  
Esau na Yakobo wakipigania urithi,  
Lakini Mungu akasema Yakobo nampenda,  
Esau ndugu wake mimi namdharau.  
  
**Uteuzi wa Mungu kweli ni wa ajabu,  
Yeye anapenda mwenye atakaye,  
Na tena anadharau mwenye atadharau,  
Namuinua sasa maana aliniteua.**

2. Mawazo yake Mungu kweli ni ya ajabu,  
Paulo akathibitisha kifo cha Stefano,  
Nguvu za uteuzi zikamjia Paulo,  
Njiani Damesiki Mungu akamuokoa.
3. Yesu kawaita mitume kumi na wawili,  
Hata kama huduma zao zilijaa maajabu,  
Yesu akafafanua sio wote wateule,  
Mmoja kati yenu ni mwana wa shetani.
4. Wateule wote kweli wanajijua,  
Asili yao yote ni ile ya Elohimu,  
Waielewa sauti ya neno ikifunuliwa,  
Lakini uzao wa nyoka kwao ni makelele.
5. Waliposulubiwa pale Kalivari,  
Mwizi upande wa ushoto akamdhihaki Bwana Yesu,  
Aliye upande wa kulia kaona dhambi zake,  
Yesu kamuokoa maana ni mteule.
6. Kitabu cha uzima kiliandikwa majina,  
Wanaouza neno wanafutwa majina,  
Kwani sehemu yao ni moto wa milele,  
Lakini Bi-arusi ni uzima wa milele.
7. Bi-arusi huyu ni wa kidhahabu,  
Watakaokolewa Israeli ni wa kifedha,  
Nao waliosaidia huyu Bi-arusi,  
Na mwanamwali mjinga hao ni wa kishaba.

## **11. BADILISHA JINA LANGU KUPITIA UFUNUO.**

1. Bwana uliponua bariki watakatifu,  
Ulibadilisha majina, tabia zao,  
Nami naja Bwana upate kunibariki,  
Ni wewe jana, leo na hata milele.  
  
**Naja Bwana ubadilisha jina langu,  
Nafsi yangu iwe nyeupe ili nikutii,  
Neno lako ufiche nafsini mwangu,  
Nidhahirisha jina lako takatifu Bwana.**
2. Abram alipashwa habari na Yehova,  
“Nitakufanya uwe baba wa mataifa,  
Ahadi yangu kwako, lazima utahiri,  
Na jina lako utaitwa Ibrahimu.”
3. Yakobo alijawa na hofu na uwoga mwingi,  
Usiku huo akakutana na malaika,  
Kabarikiwa na kuitwa Israeli,  
Mfalme aliye na ushindi mbele za Mungu.
4. Simoni alipofunuliwa Yesu ni nani,



Jina lake alibadilishwa kuwa Petro,  
Funguo za ufalme nazo pia akapewa,  
Kanisa la Yesu sasa ni la ufunuo.

5. Bwana alipoanza kufunua mihuri,  
Nabii alibadilisha jina la kanisa,  
Akatuia Bi-Arusi wa Yesu Kristo,  
Kwani Yesu anamimina uhai wake.
6. Umepokea jina jipya la Yesu Kristo?  
Maisha yake uweze kuyadhihirisha,  
Kuja upokee Jina Jipya la Yesu Kristo,  
Hili ndilo linaturudisha nyumbani.

## **12. UFUNUO WA MBEGU CHINI YA MUHURI WA SABA**

1. Hizi ndizo nyakati za mwisho,  
Mbegu iliyopandwa imerejeshwa,  
Yesu alisema neno ndilo mbegu,  
Bi-arusi sasa ameipokea.  
  
**Niko ndani ya ufufuo wa mbegu,  
Uhai wa Kristo unadhihirishwa  
Mbegu inakaushwa na jua,  
(Ili ipelekwe ghalani mwa Mungu) x2**
2. Uhai umehama kapini,  
Na umesanywa ndani ya mbegu,  
Uridhi wote pia umesanywa,  
Mbeguni, nayo kapi ichomwe.
3. Umbo la kapi ni kama la mbegu,  
Lakini tabia hazifanani,  
Kapi hutumia akili zake,  
Lakini mbegu ina "Bwana asema."
4. Huyu Mariamu alipokea mbegu,  
Yesu mkombozi akadhihirishwa,  
Sasa Bi-arusi ana hiyo mbegu,  
"Shetani sasa ujichunge sana."
5. Mbegu ilikuwa ndani ya Baba zetu,  
Hili neno likiwa mwilini,  
Ahadi ni kwamba mbegu hiyo tena,  
Itadhihirishwa nyakati za mwisho.
6. Ufunuo wa mbegu umefichwa,  
Chini ya mvuto huu wa tatu,  
Wanyama wote wanatazamia,  
Hata dunia, mbegu idhihirishwe.
7. Hiyo mbegu ni ya Ngurumo saba,  
Chini ya muhuri huo wa saba,

Nabii akasema huo ufufuo,  
Utarejesha Bi-arusi nyumbani.

## **13. ABUDU MWANA-KONDOO MKOMBOZI**

1. Nitaimba wimbo mpya nikimsifu,  
Mwana Kondoo kwa nguvu na uwezo wake,  
Alistahili kuwa mkombozi wa jamaa,  
Alipofufuka na sasa ninaimba.

**Wastahili kusifiwa Mwana Kondoo,  
Wastahili kuinuliwa Mkombozi,  
Wastahili kusujudiwa Bwana wangu,  
Ulipokufa, damu imenikomboa.**

2. Yohana akiwa kisimani cha Patmo,  
Alionyeshwa ono la kipekee,  
Walio dunia na mbingu pamoja,  
Ijulikane ni nani mkombozi.
3. Elohimu akiwa kitini cha enzini,  
Kitabu kiliwekwa mkononi mwa kulia,  
Na mihuri saba imekizunguka,  
Ikingojea kuvunjwa na mkombozi.
4. Malaika aliye na nguvu akauliza,  
"Nani anayestahili afungue kitabu?  
Tena avunje hiyo mihuri yote saba?"  
Hakuna aliyeonekana, Yohana akalia.
5. Mzee mmoja wa wale ishirini na nne,  
Akamsihi Yohana awache kulia,  
Maana Simba wa Yuda, shina la Daudi,  
Ameshinda na mihuri atavunja.
6. Ilikuwa wimbo mpya wa ukombozi,  
Mwana kondoo alipochukua kitabu,  
Tukapata tumaini la uzima,  
Mihuri ikafunua urithi wangu wote.
7. Tutawaita wale waliolala,  
Nasi tulio hai miili igeuzwe,  
Tukutane karamuni mwa Bwana Yesu,  
Avunjapo mihuri tena tutaimba.

## **14. MAHALI TEULE PA IBADA YA KRISTO YESU**

1. Mungu alipomuumba mwanadamu,  
Alimuumba na nafsi ndani yake,  
Akamfunulia mahali pa kuabudia,  
Na ni ndani ya Jina lake Bwana Yesu.



**Nafsi yangu ina amani tele,  
Kwa kuwa Yesu yeye yu ndani yangu,  
Mimi ndani Yake na Yeye ndani yangu,  
Nitamsifu Muumba wangu milele.**

2. Hapo mwanzo Roho wa Umilele,  
Tena ndiye El-Elah-Elohimu,  
Alipojinyosha mwili ukadhihirishwa,  
Ulio na Jina lake na ndiye Neno.
3. Hilo Neno lilipoumba mbiguni,  
Tena dunia na vitu vilivyomo,  
Alipowaumba Malaika na wakamwabudu,  
El-Elah-Elohimu akawa Mungu
4. Solomoni alipojenga hekalu,  
Jina la Bwana likaja na utukufu,  
Watakatifu walipopatwa na shida,  
Wakitazama hekalu wanakombolewa.
5. Yesu alipobebwa na mwana punda,  
Walifunuliwa analo Jina la Mungu,  
Wakamsifu akienda Yerusalemu,  
Kwa sauti "Hosana mwana wa Daudi."
6. Yesu alipolipa deni Kalvari,  
Wanafunzi wakajazwa na Roho wake,  
Wakapokea Jina lake Bwana Yesu,  
Wakasikika wakimsifu Muumba.
7. Baada ya mihuri saba kuvunjwa,  
Bi-arusi amepokea Jina hilo,  
La Yesu Kristo, na sasa ana uwezo,  
Wa kuumba dunia nyingine na kuishi.
8. Mahali mzoga unapopatikana,  
Wanatai wanakutana hapo wote,  
Bwana unisaidie kuishia Jina lako,  
Nibadilishe eneo ninyakuliwe.

## **15. SAUTI YA MALAIKA MKUU NDANI YANGU**

1. Baada ya malaika kuumbwa mbinguni,  
Wakamwabudu Mungu wa Umilele,  
Lucifa alipofanywa mtawala wao,  
Alijiinua awe kama Mungu.

**Nia yangu Yesu amejitwalia,  
Hamu ya dhambi ameniondolea,  
Sauti ya Malaika yule mkuu,  
I ndani yangu ewe Bwana uniongoze.**

2. Lucifa na wenzake wakafukuzwa,  
Mbinguni na Mungu aliye na wivu,  
Mbinguni kukawa na kilio kingi,  
"Woi! Woi! Vita vimeshuka dunia."
3. Baada ya kuumba Adamu na Hawa,  
Akawaweka shambani la Edeni,  
Akawapa neno lake waliishie,  
Hawa akaasi giza ikajaa dunia.
4. Adamu wa mwisho alidhihirishwa,  
Mwanadamu alipomuasi Mungu,  
Akaagikwa msalabani Kalvari,  
Deni yote ya dhambi akatulipia.
5. Moto wa Roho ukitakasa nafsi zetu,  
Huyo Malaika anaingia ndani,  
Anajitwalia nafsi na roho zetu,  
Hata miili yetu Yesu adhihirike.
6. Sauti ya Malaika huyo mkuu,  
I ndani ya Yesu kwa ukamilifu,  
Lazaro akiwa kaburini siku nne,  
Yesu alimwita naye akafufuka.
7. Yesu alipopaza sauti Kalvari,  
Tetemeko la ardhi likaonekana,  
Makaburi yakatoka watakatifu,  
Yesu alipofufuka wakaonekana.
8. Malaika aliyeshuka toka mbinguni,  
Akajifunua kupitia Branham,  
Naye akafunua mihuri yote saba,  
Bi-arusi anao uhai wa Yesu.
9. Bi-arusi anayo sauti yake,  
Malaika mkuu kwa ukamilifu,  
Tuite waliolala ardhi itetemeke,  
Wafufuke twende pamoja nyumbani.

## **16. DEEPER DEEPER**

1. Deeper, deeper in the love of Jesus,  
Daily let me go,  
Higher, higher in the school of wisdom,  
More of grace to know.

**O deeper yet, I pray,  
And higher every day,  
And wiser blessed Lord,  
In thy precious Holy Word.**

2. Deeper Deeper! Blessed Holy Spirit,  
Take me deeper still,



Till my life is wholly lost in Jesus,  
And his perfect will.

3. Deeper, deeper! Tho' it cost hard trials,  
Deeper let me go!  
Rooted in the Holy love of Jesus,  
Let me fruitful grow.
4. Deeper, higher! Every day in Jesus,  
Till all conflict past,  
Finds me conqueror and in His own Image,  
Perfected at last.

### **17. FATHER LET THE FIRE FALL**

Father let the Fire fall,  
Father let the Fire fall,  
Let the Fire fall,  
Let the Fire fall,  
Let the Pentecostal Fire fall.

Father let the glory fall,  
Father let the glory fall,  
Let the glory fall,  
Let the glory fall,  
Let the Pentecostal glory fall.

Father let the Spirit fall...  
Father let the Power fall...  
Father let the Showers fall...

### **18. COME BY HERE**

**Come by here Lord,**  
**Come by here,**  
**Oh Lord, come by here** } x3

- Someone's praying Lord...
- Someone's crying Lord...
- Someone's calling Lord...
- Someone's hurting Lord...
- Someone's singing Lord...
- How we need you Lord...
- For your presence Lord...
- You are welcome Lord...
- How we love you Lord...
- Speak to me my Lord...
- I am listening Lord...
- Lead me now my Lord...
- Bless me now my Lord...

### **19. MINE MINE MINE**

Mine, mine, mine, Jesus is mine,  
Mine, mine, mine, Jesus is mine,

Jesus is my Saviour, day by day,  
Mine, mine, mine, Jesus is mine,

### **20. FIRE FIRE FIRE**

Fire, Fire, Fire } x2  
Fire, fall on me }

As on the day of Pentecost,  
Fire fall on me,  
As on the day of Pentecost,  
Fire fall on me.

Spirit, Spirit, Spirit...  
Power, power, power...

### **21. WHAT A MIGHTY GOD**

What a mighty God we serve,  
What a mighty God we serve,  
Angels bow before Him,  
Heaven and earth adore Him,  
What a mighty God we serve.

### **22. LEARNING TO LEAN**

Learning to lean, learning to lean  
Learning to lean on Jesus,  
Gaining more power,  
Than I'd ever dreamt,  
Learning to lean on Jesus.

### **23. THIS IS THE DAY**

This is the day, this is the day,  
That the Lord has made,  
That the Lord has made,  
We will rejoice, we will rejoice,  
And be glad in it, and be glad in it.

This is the day that the Lord has made,  
We will rejoice and be glad in it.  
This is the day, this is the day  
That the Lord has made.

### **24. HALLELUYAH**

**Hallelujah, hallelujah, hallelujah,**  
**Hallelujah, hallelujah, hallelujah,**  
**Hallelujah, hallelujah,**

Lord we love You...  
You are Holy...  
You are Mighty...  
We adore You...  
Lord we praise You...



## **25. IN THE NAME OF JESUS**

In the Name of Jesus, in the Name of Jesus,  
We have the victory,  
In the Name of Jesus, precious Name of Jesus,  
Demons will have to flee.

When we come in the Name of Jesus,  
Tell me who can stand before,  
In the precious Name of Jesus,  
We have the victory.

## **26. I'M GLAD JESUS SET ME FREE**

(I'm so glad; Jesus set me free) x3  
I'm singing glory, halleluya, Jesus set me free,

I'm so glad Jesus lifted me...  
The Devil had me bound,  
But Jesus set me free...  
I'm on my way to heaven,  
Shouting victory...

## **27. THE ORIGINAL LIFE**

1. God's attributes were manifested  
To His Bride in this last day,  
We have caught the revelation,  
By the last prophet's message;  
And we know who we are,  
And what we are raised up for,  
Praise the Lord for the Original Life.

**The Original Life, the Original Seed,  
The Original Word is what I believe,  
The Son of Man is revealed;  
The Seventh Seal is unveiled,  
The Original Life, the Original Seed.**

2. Our eyes of understanding,  
He has opened up at last,  
And sweet victory is ours,  
Who were chained down in the past;  
True jubilee has sounded,  
And we have responded to our God,  
Who's the Original Life.
3. We are the word made flesh today  
This is what the scripture say  
And our names are seen within,  
Redeemed and perfect without sin;  
Yes we are anointed and inspired  
By our God, Who's the Original Life.

4. We are called unto adoption,  
Full authority and power,  
Sleeping saints will wake and join us,  
For translation in this hour;  
Gentiles' days soon be over,  
Glory, Hallelujah!  
To our God, who's the Original Life.

## **28. WE ARE MARCHING OVER**

(We are marching over to Jerusalem.) x2  
(Jerusalem, Jerusalem) x2

-To the body change  
-Into theophany  
-To the marriage feast  
-To millennial reign  
-To eternity

## **29. SEE YOU IN THE RAPTURE**

1. If we never meet again  
On this earth, my precious friend,  
If to God you have been true,  
And we've lived above all sin,  
Then for us there'll be a greeting,  
For there's going to be a meeting,  
I'll see you in the rapture,  
Some sweet day.

**I'll see you in the rapture,  
See you in the rapture,  
See you at that meeting in the air,  
There with our blessed Saviour,  
We'll live and reign forever,  
I'll see you in the rapture,  
Some sweet day.**

2. To my loved ones let me say,  
That there'll surely come a day,  
When the Lord will come again,  
And He'll take his Bride away,  
Do get ready now to meet Him,  
And with halleluyahs greet Him,  
I'll see you in the rapture,  
Some sweet day.

## **30. BY HIS WORD**

1. It is written that man shall not live  
by bread alone  
But by every word that comes from  
the mouth of God  
And by his word he gave His son  
for us on Calvary



To pay the price of sin for you  
and for me

**By His word**

**He raised the sick man from the bed**

**By His word**

**He gave life unto the dead**

**By His word**

**He brings hope to the hopeless soul**

**By His word**

**You can have the victory**

**By His word**

**He will set the captive free**

**By His word**

**He brings life to you and me**

2. Just one word was broken in Eden  
And that's what caused the fall  
So it will take all of the word  
To bring us back to God  
And through this last day message  
All His word has been made known  
And through His power we shall  
Overcome

**By His word**

**He spoke and squirrels did appear**

**By His word**

**Storm go back from where you came**

**By His word**

**Little fishy I give you back your life**

**By His word**

**He spoke the tumor out of existence**

**By His word**

**He gave two boys salvation**

**By His word**

**He gave life to you and me**

### **31. BI-ARUSI AMEBARIKIWA NA BARAKA**

#### **ZOTE ZA KIROHO**

1. Niko mbele yako Bwana (Ili unibariki) x2  
Ewe Mungu wangu

**(Ahadi zako Baba ni za kweli zote,  
yale umenijalia, na yaliyosalia,  
ninakungojea) x2**

2. Huyo roho wa tai,  
Neema yako Bwana,  
Ushirika wako Bwana,  
Ufunuo wako Bwana. } (Wewe ulinijalia) x2  
Ewe Mungu wangu

3. Nuru ya jioni,  
Imani ya Baba zetu,  
Imani ya unyakuzi,  
Nia yako Bwana. } (Umenifunulia) x2  
Ili unibariki
4. Neno la wakati,  
Nayo Malaki nne,  
Ufunuo kumi,  
Mihuri saba } (Umenifunulia) x2  
Ili unibariki
5. Kujiulewa kwangu,  
Bibi yangu mpenzi,  
Bwana wangu mpenzi,  
Watoto watiifu } (Wewe ulinijalia) x2  
Ewe Mungu wangu
6. Kuadhimishwa kwangu,  
Neno la kunena,  
Kunena wokovu,  
Ukamilifu wako. } (Uliniahidi) x2  
Ewe Mungu wangu
7. Arusi ya Mwana Kondoo,  
Neno kuwa mwili,  
Kutoonja Mauti,  
Kuita waliolala. } (Uliniahidi) x2  
Ewe Mungu wangu
8. Kugeuzwa mwili wangu,  
Kurejeshwa ujana,  
Kuvikwa kanzu nyeupe,  
Kubadilisha eneo. } (Uliniahidi) x2  
Ewe Mungu wangu
9. Karamu ya Mwana Kondoo,  
Taji ya utukufu,  
Utawala miaka elfu ,  
Kuingia Yerusalemu. } (Uliniahidi)x2  
Ewe Mungu wangu

### **32. MAJINA SABA YA UKOMBOZI**

1. Bwana wangu wewe unanijua,  
Hata giza likizidi dunia (Bwana),  
Ulinipa wokovu wako Bwana,  
Wewe ndiwe Yehova-Yire.

**Nafsini mwako nitajificha,  
Niabudu Jina lako Bwana, (wangu)  
Lililo Jipya na Takatifu,  
Nimiliki ukombozi wangu.**

2. Majaribu na taabu nyingi sana,  
Huondoa amani nafsini (mwangu),  
Ujapo unarejesha amani,  
Ni wewe Yehova-Shalomu.





3. Magonjwa yanaponisonga sana,  
Hutazama msalabani mwako (Bwana),  
Kwa mapigo yale uliyoyapata,  
Yehova-Rapha unaniponya.
4. Nafsi yangu ikiwa na njaa nyingi,  
Ya neno lako ewe Bwana (wangu),  
Malishoni ya majani mabichi,  
Yehova-Raah unanilaza.
5. Adui zangu wanaponiinukia,  
Macho yangu nakuinulia (Bwana),  
Vita vyote unanipigania,  
Wewe ndiwe Yehova-Nissi.
6. Ni ahadi yako nisiwe na hofu,  
Kila siku utaandamana (nami),  
Niendapo na nirudipo Bwana,  
Wewe ndiwe Yehova-Shammah.
7. Roho wako ulinijaza nafsi,  
Haki yako niwe nayo Mungu (wangu),  
Niweze kulitii neno lako,  
Wewe ndiwe Yehova-Tsidkenu.

### **33. MATENDO YAKO**

1. Matendo yako kweli ni ya ajabu,  
Kutoka hapo mwanzoni,  
Hujawahi badilika Yesu,  
Hakuna jambo linakushinda.  
  
**Tumfuatani (Elohimu), x2  
Hadi sote tukamilishwe,  
Yeye anazo baraka zetu,  
Lolote hatuwezi bila yeye.**
2. Amefunulia Bi-arusi wake,  
Hiyo ahadi ya Malaki nne,  
Kurejesha imani ya Baba zetu,  
Wakati huu wa omega.
3. Nabii wa wakati amedhihirishwa,  
Ngurumo saba zikafunuliwa,  
Zikafunua neno lililofichwa,  
Mimi na wewe jibu la wakati.
4. Ndugu na dada omba Roho wa Mungu,  
Uogele kisimani hai,  
Hapo kunao ule unyakuzi,  
Ahadi zake ni za kweli.
5. Bi-arusi anao unyakuzi,  
Uponyaji pia amemiliki,

Tena kuita wetu waliolala,  
Huyu Bi-arusi ni wa ajabu.

### **34. NATAMANI KURUDI NYUMBANI**

1. Shamba la Edeni lilikuwa na utulivu,  
Adamu na Hawa wakiishi umileleni,  
Urithi wa Mungu wote waliumiliki,  
Hawa kadanganywa giza likaingia dunia.  
  
**Nitimizie ahadi Yesu ulizoniahidi,  
Dunia ya giza niiondoke Mkombozi,  
Nina kiu nafsi niingie Umilele,  
Ni dhahiri Bwana natamani rudi nyumbani.**
2. Elohimu Muumba akijawa na upendo,  
Akajivika mwili wa damu na nyama,  
Aliposulubiwa deni akalipa yote,  
Nafsi yangu sasa i ndani ya Umilele.
3. Muhuri wa saba pale ulipofunuliwa,  
Malaika mkuu akaonekana akishuka,  
Alipotoa sauti ya simba angurumaye,  
Ngurumo saba zikaufunua Umilele.
4. Viumbe vyote vimeishi vikiugua,  
Wana wa Mungu waweze kudhihirishwa,  
Sababu Umileleni hakuna kudhulumu,  
Wala kuharibu natamani rudi nyumbani.
5. Hakuna kilio na shida Umileleni,  
Pia uchungu na kifo ni yaliyopita,  
Vazi jeupe halitaharibika milele,  
Niwazapo haya natamani rudi nyumbani.
6. Mitume, Ireneo na Martin waliingia,  
Mji huu kwa huyo Roho wa Simba,  
Nao Columba na Thiatira wakaingia  
Mji huu kwa huyo Roho wa Ndama.
7. Luther, Wesly na Pentekoste waliingia,  
Mji huu kwa huyo Roho wa Mwanadamu  
Nasi tulio kanisa la Omega,  
Twaingia mji kwa Roho wa Tai.
8. Utukufu wa Mungu uko Yerusalemu,  
Elohimu ndiye nuru ya mji huo,  
Njia za dhahabu na madini ya dhamani,  
Yemejenga huo mji, natamani nyumbani.

### **35. TUASHENI TAA ZETU**

1. Tuasheni taa zetu,  
Maana giza linaja,  
Giza kubwa duniani,



Taa zetu natuashe.

**Kwa upendo mwingi sana,  
Tuasheni taa zetu,  
Bwana wetu yuashuka,  
Taa zetu natuashe.**

2. Wengi mno sasa hivi,  
Mioyoni wamelala,  
Sisi nasi twaamini,  
Bwana wetu yuaja.
3. Neno lake ndilo taa,  
Na tusidanganyike,  
Hatari japo ni nyingi,  
Bwana hatatuacha.
4. Kwa maisha ya imani,  
Adui wanashindwa,  
Baraka tele kwa kutii,  
Shaka zikiondoka.

### **36. BI-ARUSI AMEZUKIWA NA JUA LA HAKI**

1. Tunafuraha kwa ajili ya Baba Elohimu,  
Siri zake zote yeye ametufunulia,  
Kwa kuzukiwa na Jua tumejijua,  
Tunacheza-cheza kama ndama kwa ukombozi.

**Tumefahamu kwa kuzukiwa na Jua la Haki,  
Tulitoka kwa Yehova Baba wetu wa mbinguni,  
Sisi balozi wa mbinguni humu duniani,  
Tunacheza-cheza kama ndama kwa ukombozi.**

2. Gorofani mitume walikuwa na nia moja,  
Jua la haki likazukia nafsi zao,  
Nafsi zao zikapokea Roho wa Mungu,  
Wakacheza-cheza kama ndama kwa ahadi.
3. Jua la mashariki sasa liko magharibi,  
Ufunuo wa Ngurumo saba tumepokea,  
Tumefanyika haki yake yeye Mungu,  
Tunacheza-cheza kama ndama mbele yake.
4. Uzao wa nyoka ukizukiwa na Jua,  
Huteta hili Jua limekuwa kali sana,  
Na kwenda gizani totoro lile la madhehebu,  
Wakidai siku za miujiza zote zilikwisha.
5. Jua la haki likizukia nafsi zetu,  
Tunadhihirisha rangi saba za upinde,  
Kama koti la Yusufu lenye rangi saba,  
Mungu anatukuka ukamilifu ukidhihirishwa.

6. Na tuamke nuru yetu sasa imekuja,  
Bi-arusi wa Mwana Kondoo wa Mungu ni sisi,  
Tujivike imani ile ya mababa zetu,  
Tuite waliolala sote twende nyumbani.
7. Tutakapoingia hilo eneo la saba,  
Tukutane na Yesu Kristo aliyetufia,  
Tukijua dhiki za dunia zimekwisha,  
Tutacheza-cheza kama ndama Umileleni.

### **37. UBATIZO WA MAJI KWA JINA LA BWANA YESU KRISTO WAKATI HUU**

1. Malachi nne ilipotimia mihuri saba,  
Ikavunjwa na kumfunua huyu Elohimu,  
Na tabia yake ya kubadilisha kinyago,  
Tunabarikiwa anapolifunua Jina lake.

**Katika Jina takatifu la Bwana Yesu Kristo,  
Tunabatizwa kwalo, na kufa pamoja naye,  
Na tunafufuka naye Yesu mkombozi wetu.**

2. Mungu Baba alikuwa juu ya Waisraeli,  
Naye akajivika mwili wa damu na nyama,  
Akawa Mwana wa Mungu na akalipa deni,  
Akaja nafsi zetu tena akiwa Roho.
3. Yohana alikuwa sauti iliao nyikani,  
Nafsi zitayarishwe kumpokea mkombozi,  
Majini mengi akawa na ubatizo wa toba,  
Alipobatiza Yesu, kafara ikatakaswa.
4. Yesu alipofufuka akawaagiza mitume,  
Waenende wawafanye mataifa wanafunzi,  
Wakiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana,  
Na Roho na ndilo Jina la Bwana Yesu Kristo.
5. Roho mtakatifu aliposhukia mitume,  
Petero, akawaambia Waisraeli wabatizwe,  
Katika Jina pekee, Bwana Yesu Kristo,  
Paulo akabatizana pia kama wengine
6. Tukibatizwa katika Jina la Bwana Yesu,  
Tunajiunga katika ushirika wa waaminio,  
Tunalilia Mungu atuzae na Roho wake,  
Tunazaliwa ndani ya mwili wa Yesu Kristo.
7. Bi-arusi amebatizwa katika Jina hilo,  
Amepokea Roho aliye kama Tai,  
Amejivika Jina lake Bwana Yesu Kristo,  
Tunatawala pamoja naye Yesu Kristo.





8. Roho wa Mungu amesema tufanye mambo yote,  
Katika Jina lake Bwana Yesu Kristo,  
Ubatizo wa maji hata na ule wa Roho,  
Pia tunyakuliwe ndani ya Jina hilo.

### **38. JINA LANGU LAITWA CHINI YA MUHURI WA SABA**

1. Mwana-kondoo Yesu msalabani akaangikwa,  
Mwanzoni kabla Mungu hajaumba dunia,  
Kitabuni chake majina yakaandikwa,  
Ya watakatifu kwa damu yake Yesu,

**Jina langu sasa, na linaitwa,  
Hizi Ngurumo saba na ziliapo,  
Limeandikwa chini ya muhuri wa saba,  
Langu jina linaitwa nitwae urithi wangu.**

2. Mwanamke msamaria alipambanuliwa,  
Nafsi yake na Yesu hapo kisimani,  
Akajua yeye ndiye Kristo wangojea,  
Akaliona jina lake kitabuni.
3. Yesu aliwauliza hao mitume wake,  
Yeye ni nani Petro akajibu,  
Wewe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai,  
Akaitika jina lake kitabuni.
4. Kwa ufunuo wa haki Luther akaitika,  
Naye Wesley akaitika kwa utakaso,  
Pentekoste kwa vipawa wakaitika,  
Ngurumo saba ziliapo ninaitika.
5. Bi-arusi ajielewa jina likiitwa,  
Tukipokea ukamilifu wake Yesu,  
Tudhihirishe nguvu za Mungu za umbaji,  
Tuite waliolala sote twende nyumbani.

### **39. KUTEMBEA NA ELOHIMU NIKAMILIKE**

1. Kwa kuvunjwa kwa muhuri huo wa saba,  
Urithi wangu naona ukifunuliwa,  
Nitatembea nawe hatua kwa hatua,  
Nikamilike ili nikudhihirishe.

**Mimi ninatamani kutembea nawe,  
Nifanane nawe Yesu unipendaye,  
Nikudhihirishe nifananapo nawe,  
Hebu nitembee nawe uninyakue.**

2. Nitatembea na wewe Elohimu,  
Kama vile Enoko alitembea nawe,

Baada ya Methuselah kuzaliwa,  
Kwa kutembea nawe ukamnyakua.

3. Nitatembea nawe kama Elija,  
Ishara na maajabu yakaonekana,  
Imani ya kunyakuliwa akaipokea,  
Kwa farasi za moto akaenda nyumbani.

4. Nabii Branhamu alitembea nawe,  
Msituni ule wa Colorado,  
Ukamuonjesha ujana wa Umilele,  
Ikawa thibitisho nitabadilishwa.

5. Bi-arusi akitembea na Elohimu,  
Anajivika neno awe neno la kunena,  
Tena tujivike imani kamilifu,  
Tuite waliolala tunyakuliwe.

### **40. UKOMBOZI WETU WADHIHIRISHA UTUKUFU WA MUNGU**

1. Hapo mwanzo Elohimu aliwazia,  
Jinsi ya kuwa Mungu wa kuabudiwa,  
Ndani yake alijawa na sifa nyingi,  
Kwanza akaumba Malaika na kumuabudu.

**Sitaacha kukusifu Mungu wangu,  
Sifa ndani yako umezifunua,  
Nikudhihirishe, humu duniani,  
Hata ukininyakuwa nitakusifu.**

2. Tuliitoka mawazoni ya Elohimu,  
Tukaipita miili yetu ya Neno,  
Tukavikwa miili ya nyama na damu,  
Wetu uasi, ukombozi ukafunua sifa.
3. Mungu Muumba akijua mambo yote,  
Kampa mwanadamu neno akaasi,  
Elohimu kafanyika mwokozi wetu,  
Sifa zake nyingi zikadhihirishwa.
4. Kwa sababu ya kukosa ufunuo,  
Shetani alimuangusha mwanadamu,  
Ndipo Yesu Kristo akasulubiwa,  
Na yeye ndiye Mwokozi na Mkombozi.
5. Sifa zake zi ndani ya Bi-arusi,  
Kiti cha rehema pia ndani yetu,  
Tunene wokovu pia uponyaji,  
Umbaji tuonyeshe na tujinyakue.
6. Tukibadilisha eneo malaika,  
Watatazama tukisifu Mwana Kondoo,  
Tukiimba wimbo mpya wa ukombozi,



Tukisema nguvu na uweza ni zake.

#### **41. UKINGONI MWA YORDANI**

1. Ukingoni mwa Yordani,  
Kumeandaliwa,  
Bara zuri la Zayuni,  
Ninalotamani.

**Tutakaa pamoja na Yesu,  
Katika pwani yenye raha,  
Tutaimba wimbo wa Mwana Kondoo,  
Milele hata milele.**

2. Bara hilo kuna nuru,  
Nuru ya milele,  
Kristo Jua huangaza,  
Hufukuza giza.
3. Mji huo mu bustani,  
Tutapumzikia,  
Tena mto wa uzima,  
Kama kioo hung'aa
4. Nitayafikia lini,  
Na kunyakuliwa,  
Kwenye ufalme wa Baba,  
Na kumwona uso.
5. Furaha yangu Moyoni,  
Ni kunyakuliwa,  
Sitaogopa mawimbi,  
Katika Yordani.
6. Arusi ya Mwana Kondoo,  
Imeandaliwa,  
Bi-arusi amevikwa nguo,  
Nguo ndiyo Neno.

#### **42. UNYAKUZI WA BI-ARUSI KWENDA KARAMUNI**

1. Kwa utimilifu wa Malaki nne,  
Ufunuo kumi tumejitambua,  
Kwamba tulitoka ndani ya Elohimu,  
Baada ya ukombozi tutaishi naye.

**Ninakuomba ewe Elohimu,  
Nafsi yangu neno lako litawale,  
Yako ghadhabu ukutilia dunia,  
Niwe nawe Yesu huko angani.**

2. Tukinyakuliwa mwanamwali mjinga,  
Atawindwa na kuawa na mnyama,

Sababu ufunuo tuliopokea,  
Umefunua Shetani na hila zake.

3. Waisraeli watajitambua,  
Musa na Eliya wakiinuliwa,  
Wamjue Yesu waliyemsulubisha,  
Walie wakijuta "tulifanya nini."
4. Uzao wa nyoka umejaza kikombe,  
Na uovu wao tayari kwa hukumu,  
Yale mapigo saba Mungu awachilie,  
Wachomwe na moto na wawe majivu.
5. Baada ya Shetani kujiinua dunia,  
Na kuingia hekalu ili aabudiwe,  
Mundu wa Yehova u mkononi mwake,  
Mnyama achomwe pia mji wake.
6. Tutapewa taji huko angani,  
Sisi tu wafalme pamoja na Kristo,  
Tumvike Yesu taji ya utukufu,  
Akiwa Mfalme wa Wafalme wote.

#### **43. GOD WILL MAKE A WAY**

God will make a way,  
Where there seems to be no way,  
He works in ways we cannot see,  
He will make a way for me,  
He will be my guide,  
Hold me closely to His side,  
With love and strength for each new day,  
He will make a way...  
He will make a way...

#### **44. CAN'T YOU SEE WHY I AM SO HAPPY**

Can't you see,  
Why I am so happy,  
I have accepted the Word of the Lord,  
The revealed Word that was spoken,  
By the prophet of Malachi 4

#### **45. JESUS IS THE WINNER MAN**

Jesus is the winner man,  
A winner man, the winner man,  
Jesus is the winner man,  
The winner man all the time.

Satan is a loser man,  
A loser man, a loser man,  
Satan is a loser man,  
A loser man all the time.



I am on the winning side,  
The winning side, the winning side,  
I am on the winning side,  
The winning side all the time.

#### **46. ELIEZER'S CAMEL TRAIN**

1. Twas a day in early spring time,  
By an ancient wayside well,  
Eliezer paused to rest his camel train,  
He had found a Bride for Isaac,  
As the evening shadows fell,  
And his weary journey had not been in vain.

**O get ready, the evening shadows fall,  
Don't you hear that Eliezer call?  
There's going to be a wedding supper,  
Our joys will soon begin,  
In the evening when the camel train comes in.**

2. So he took the fair Rebekah,  
Decked in jewels rich and rare,  
Back to Abraham and Isaac far away,  
Now Rebekah loved her Isaac,  
And he loved Rebekah fair,  
Oh it must have been a happy wedding day.
3. The blessed Holy Spirit,  
Through the prophet of this day,  
Has come down to earth to claim a worthy Bride,  
For our Isaac over yonder,  
Has prepared His tents of love,  
And he wants His fair Rebekah by His side.
4. We've left our kinfolks gladly,  
We've bade the world goodbye,  
For we're going to a land beyond the sky,  
We shall soon behold our Isaac,  
In the blest Eternity,  
What a happy, happy meeting that will be.

#### **47. HUKUMU BAADA YA KARAMU NA MIAKA ELFU**

1. Tutokapo hiyo karamu ya Bwana,  
Tutawale naye miaka elfu moja,  
Uzao wa nyoka watakuwa kuzimu,  
Tumekombolewa shetani atafungwa dunia.

**Sinayo shaka kifoni nimetoka,  
Na kujivika Kristo Mkombozi wangu  
Haki yake ninayo dunia ni ihukumu,  
Wazuri kwa wabaya niwatenganishe.**

2. Utawala miaka elfu moja ukiisha,  
Wafu wote na wafufuliwe,  
Kuwe na vita naye Mungu aizime,  
Kitini cheupe cha hukumu wasimame.
3. Kama mchungaji anavyozitenganisha,  
Kondoo zake kwa mbuzi zake,  
Yesu akiwa kitini cha hukumu,  
Wenye haki uzimani mbuzi atupe motoni.
4. Walio wake Mungu atawatukuza,  
Wale dunia iliyowadharau,  
Wasiotii neno lao la wakati,  
Watalia wakisumbuka huko motoni.
5. Moto ukitakasa dunia hii,  
Mji wa Yerusalemu utashuka,  
Maisha ya Kristo sasa tunayoishi,  
Yamejenga mji huo tutaishi naye.

#### **48. MEZA YA BWANA**

1. Meza ya Bwana iliyotakatifu,  
Tai twakusanyika hapo kama ishara,  
Ya ushirika naye Bwana Yesu Kristo,  
Tunaishi kwa mwili na damu hiyo yake.

**Yesu aliubariki mkate na kuumegea,  
Mitume wakaula mfano mwili wake,  
Kikombe cha divai tena akakibariki,  
Wakainywa damu ya agano lililo jipya.**

2. Ujihoji ndugu, ujihoji dada,  
Maisha yake Kristo unayadhihirisha?  
Tubu dhambi zako kama hudhihirishi,  
Baraka zake Mungu utazipokea.
3. Yesu akawaambia hao mitume wake,  
Yeye ndiye mkate utokao mbinguni,  
Na yeye alaye ataishi milele,  
Uweza wa kifo haumo juu yake.
4. Mwana Kondoo aliangikwa msalabani,  
Akasema nguvu za dhambi zimekwisha,  
Ukombozi mkamilifu urithi wangu,  
Nitaishi kumsifu Mwokozi wangu.
5. Yesu usiku huo akawaambia mitume,  
Hatakunywa tena uzao wa mzabibu,  
Hadi wakutane karamuni Mwake,  
Tukinyakuliwa sote huko hewani.
6. Muhuri wa saba ulipofunuliwa,  
Mkate wa uzima tumemegewa,



Neno la asili liko ndani yetu,  
Tuonyeshe ukamilifu wake twende nyumbani.

#### **49. MIMI NI MSAFIRI**

1. (Mimi ni msafiri) x2  
Naenda juu Zayuni  
Njiani ninaimba  
Nasifu mwokozi Yesu } x2
- (Na sasa mi mshindi) x3  
**Kwa nguvu za Yehova**  
**Jemedari wanishika** } x2
2. (Nilikuwa mtumwa) x2  
Kifungoni mwa shida  
Yesu naye kaivunja  
Minyororo yake shetani } x2
3. (Hata niwe nyikani) x2  
Sitapatwa na kiu  
Maana chemchemi  
Zatoka ndani yake Yesu } x2
4. (Walisema sishindi) x2  
Wakasema mi bure  
Mpenzi kanijuza  
Atanipa wake uzima } x2
5. (Bwana alinitoa) x2  
Kama alivyowatoa  
Wana wa Israeli  
Toka nchini ya utumwa } x2

#### **50. KUTAWADHANA MIGUU**

1. Meza ya Bwana ilipotamatika,  
Yesu aliweka kando mavazi yake,  
Ya juu, na kiunoni kitambaa akajifunga,  
Kisha maji akatia ndani ya bakuli.  
  
**Yeye Bwana atupenda na ni mnyenyekevu,  
Miguu ya mitume akaitawadha,  
Wake uhai aliutoa ili tuokolewe,  
Tuzidi kufanya hivyo kwa Roho wake.**
2. Maji bakulini akatawadha miguu,  
Ya mitume wake, kisha na kuifuta,  
Na hicho kitambaa alichojifunga,  
Yeye Mwalimu na Bwana aliyenyenyekea.
3. Yesu alipotoka utukufuni akawa,  
Mmoja wetu na kunyenyekea kifo,  
Alipofufuka Mungu akalitukuza,  
Jina lake hadi mbingu na dunia zalitii.

4. Baada ya kuvunjwa kwa muhuri wa saba,  
Bi-arusi analo Jina jipya la Yesu,  
Tushiriki shida za walio wetu,  
Tunyenyekeane upendo wa Mungu udhihirike.

#### **51. ROHO ATANGAZA HAKUNA WAKATI** **TENA**

1. Roho yuatangaza, humu hana wakati,  
Atapaa mbinguni, apae na wapenzi,  
Wakati umefika, wa kurudi kwa Yesu.  
  
**Halleluyah e Bwana**  
**Roho utuandae**  
**Tuvike utukufu.** } x2
2. Tashwishwi na shaka, uvivu na uzembe,  
Ni mbinu za shetani, tujifunze na Yesu,  
Aliye mtulivu, hupenda na hurehemu.
3. Ghadhabu yake Mungu, itamiminwa dunia,  
Sodoma nayo ichomwe, walimwengu walie,  
Tena waangamizwe, kuja chini ya Haki.
4. Kwa Ujumbe wa sasa, Malaki nne tano,  
Ufunuo nayo kumi, yote yawezekana,  
Jisalimishe papo, utakuwa mshindi.
5. Takasa hilo vazi, Bwana Arusi yu hapa,  
Taa zetu na tuashe, kama kufumba jicho,  
Atachukua wapenzi, shida zote tuage.

#### **52. KUWEKWA WAKFU WATOTO**

1. Mitume wa Yesu waliwazuilia,  
Watoto wapelekwe kwake Bwana Yesu,  
Yesu akawakanya na kuwashauri,  
Watoto waje kwake ili awabariki.  
  
**Watu walileta watoto kwa Yesu,  
Akawachukua mikononi mwake,  
Kwa mikono yake iliyotakatifu,  
Kwa upendo mwingi yeye akawabariki.**
2. Bwana twaomba ulinde watoto hawa,  
Huyo shetani kamwe asiwadhuru,  
Tena twaomba haja zao uzitimize,  
Za maisha haya tena ya Neno lako.
3. Twaombea pia wanaolea watoto,  
Wasikasirishe Malaika wao kamwe,  
Bali wawalee kwa Neno la wakati,  
Wakijitambua wamwendee Bwana Yesu.



4. Yesu alisema ufalme wa Mbinguni,  
Unapokelewa na walio kama hawa,  
Watoto, maana ni wanyenyekevu,  
Tena wana upesi wa kumtii Bwana.
5. Malaki nne ilipotimia imefunuliwa,  
Watoto hawa ni dada na ndugu zetu,  
Katika ufalme wa Baba huyo wetu,  
Ni jukumu tumepewa la kuwalea.

### **53. WIMBO WA KUWAIMBIA WALIOPOSANA**

1. Baada ya Adamu kuumbwa na Mungu,  
Alionekana yu mpweke sana,  
Mungu akamuumba Hawa msaidizi,  
Ndiyo maana amekupa mpenzi wako.

**Mlitoka ndani yake Elohimu,  
Wakati ukapata kuwatenganisha,  
Mmefunuliwa ninyi mwili mmoja,  
Kama Yesu Kristo naye Bi-arusi.**

2. Umepewa ufunuo naye Elohimu,  
Na huyu ni mfupa wa mifupa yako,  
Tena nyama katika nyama hizo zako,  
Pia roho yake iliishi ndani yako.
3. Baada ya Neno la Mungu kukuzaa,  
Bwana amekupa kipawa kizuri,  
Bibi mwema Mungu anayepeana,  
Hakuna kitakachowatenganisha.
4. Ni dhahiri wazazi umewaacha,  
Muwe mwili mmoja naye bibi yako,  
Kwa maisha haya tena ya umilele,  
Muishi kwa utakatifu wake Yesu.
5. Muhuri wa saba sasa umefunua,  
Aposaye bibi yu sehemu yake,  
Walikuwa ndani yake Elohimu,  
Tunashuhudia leo neno hilo.

**BWANA ARUSI ANAMUIMBIA BI-ARUSI**  
Wewe u furaha ya nafsi yangu,  
U mfupa katika mifupa yangu,  
Tena u nyama katika nyama zangu,  
Roho yako pia iliishi ndani yangu.

**BI-ARUSI ANAMWIMBIA BWANA ARUSI**  
Mimi mfupa katika mifupa yako,  
Tena ni nyama katika nyama zako,

Pia roho yangu iliishi ndani yako,  
Wewe ndiwe bwana wangu maishani.

**BWANA NA BI-ARUSI WAIMBA PAMOJA**  
Tulitoka ndani yake Elohimu,  
Wakati ukapata kututenganisha,  
Tu pamoja tena humu duniani,  
Kama Yesu Kristo naye Bi-arusi.

### **54. MWILI WANGU WA NENO WANIITA**

1. Ulinivika mwili wa nyama na damu,  
Nilipotoka mawazoni Mwako,  
Nikaupita mwili wangu wa neno,  
Na sasa nasikia ukiniita.

**Mwili wangu wa neno unaniita,  
Ngurumo saba zifunuliwapo,  
Sauti ya Elohimu naisikia,  
Uniongoze ewe Bwana.**

2. Shida nyingi sana ninazipitia,  
Mwendoni mwa maisha haya,  
Ninapolemewa sauti naisikia,  
Iliyo nyororo nitashinda.
3. Ninakuomba Bwana unifananihe,  
Na mwili wangu wa neno,  
Niwe mkamilifu kama wewe ulivyo,  
Nikudhihirishe duniani.
4. Mwili wangu wa neno unanivuta,  
Nirejeshwe huko uliko mbinguni,  
Unaniandama popote niendapo,  
Na kunikemea nikosapo.
5. Sauti naisikia ya ahadi zangu,  
Nifanyike neno linenalo,  
Waliolala pia nipate kuwaita,  
Tunyakuliwe sote angani.

### **55. KUPAA KWA TAI KATIKA AHADI ZA WAKATI**

1. Mtu alipofukuzwa Edeni,  
Yesu akalipa deni ya dhambi,  
Makerubi warejeshwa  
Mtu, mtini wa uzima.

**E Bwana nakuomba,  
(nakuomba),  
Nipae kwenye ahadi (zangu),  
Kwa mabawa yangu ya tai,  
Hapo yote yanawezekana.**





2. Niliishi sijielewi,  
Nikala pamoja na kuku,  
Mama tai aliponiita,  
Nikajua mi tai na kupaa.
3. Ninapomkosea Mungu,  
Nakwenda hapo Kalvari,  
Hapo madhabahuni ya kishaba,  
Hatia naoshwa na kupaa.
4. Kwa kuvunjwa kwa muhuri,  
Wa saba, ukafunua,  
Roho wa tai awe ndani yangu,  
Nakuupokea ukombozi.
5. Mungu amenipa Roho wa tai,  
Kiti cha rehema ndani yangu,  
Ninene wokovu kwa watu wake,  
Hata viungo via mwili ninene.
6. Tukidhihirishwa sisi wana  
Wa Mungu, tuite walalao,  
Tupae sote angani,  
Tumlaki Yesu mpenzi wetu.

## **56. KUJA KWA BWANA KU NDANI YA BI- ARUSI WA KIZAZI.**

1. Tumefika kweli mwisho wa dahari,  
Mihuri yote saba imefunuliwa,  
Ishara yake Yesu imeonekana,  
Ya kuja kwake hapa mara ya pili.  
  
**Kuja kwako Bwana ukuimarische,  
Ukuimarische ndani yangu,  
Imani ya kunyakuliwa uizidishe,  
Unibadilishe mwili wangu,  
Nije huko Wewe uliko.**
2. Muhuri wa saba umefunuliwa,  
Mkate wa uzima tumeupata,  
Mwaliko wake Mfalme u ndani yetu,  
Njia ya kuondoka tumeiona.
3. Yesu atatuondoa kwa kutunyakua,  
Kama Yusufu alivyowaondoa,  
Bibi yake na watoto na kuwaficha,  
Ili ajifunue kwa ndugu zake.
4. Siku ya kuondoka humu dunia,  
Imefichwa ndani ya nafsi zetu,  
Roho mtakatifu naye atatujuza,  
Wakati wa kuondoka umefika.

5. Sauti ya Malaika aliye mkuu,  
I ndani yetu tuite walalao,  
Tarumbeta ya kwenda iko ndani yetu,  
Tubadilishe miili tena eneo.
6. Tuingiapo hilo eneo la saba,  
Tutamwona aliyetukomboza,  
Akiwa kijana kama tulivyo,  
Tutaimba halleluya tumeshinda.

## **57. WAKATI UNAISHA.**

1. Nafasi inaisha, ya Roho kuitana,  
Wakati nao uje, wa huzuni, machozi  
  
**Nalitazama neno, linapima weupe,  
Wa mioyo ya wapenzi, Roho karibu kupaa.**
2. Roho yuna kilio, kwa ajili ya mioyo,  
Iliyokataa neno, Roho karibu kupaa.
3. Na mwisho wa dahari, ndio huu tulimo,  
Mwenye hekima ajue, Roho karibu kupaa.
4. Ishara tumeona, za kurudi kwa Yesu,  
Ngurumo zimenena, Roho karibu kupaa.

## **58. NI WAKATI WA KWENDA NYUMBANI.**

1. Hii ni ahadi kwamba mwisho wa dahari,  
Mwana wa Adamu atajifunua kwetu,  
Hata uovu, uzidipo, tukamilike twende nyumbani.  
  
**(Kweli) Ngurumo saba zinatoa, } x2  
Sauti zake, twende nyumbani.**
2. Siku tulimo ni kama zile za Nuhu,  
Walijenga safina nao wengine,  
Wakala na wakanywa, Mungu akawamaliza,  
Niwezeshe nikutii Ewe Bwana.
3. Kama siku za Gomora na Sodoma,  
Uovu ulizidi Mungu akawachoma,  
Lakini Ibrahimi, yeye akarehemika,  
Wakarejeshewa ujana wao.
4. Niwezeshe Ewe Bwana nikamilike,  
Nikudhihirishe humu duniani,  
Pia wokovu niupeane,  
Kwa wapendwa na twende nyumbani.
5. Tai sasa anaongozwa na Jiwa,  
Kwenda hewani karamuni ya Bwana,  
Pia utawala wa miaka elfu moja,



Tuishi naye Yesu milele.

## **59. IBADA YA MWANAKONDOO WA MUNGU**

**Mwanakondoo,  
Sifa zake nyingi na zivume (kote),  
Kwa kuivunja mihuri saba,  
Ukombozi mkamilifu ni wangu.**

-Ni Mkombozi                -Ni mchungaji,  
-Ni Mwokozi                -Warehema  
-Ni Mponyaji               -Ni Mfariji  
-Ni Mwalimu                -Ni Mshindi

-----  
-Tumwamini                -Shangilia  
-Tumtii                        -Tumrukia  
-Tumsifu                      -Tumuinue  
-Tumwabudu                -Tumtukuze  
-Tumwimbie                -Tumnenee  
-Tumsujudu                -Twende kwake

## **60. YESU KRISTO MSAMARIA MWEMA.**

1. Ni hapo shambani hilo la Edeni,  
Urithi wangu nilipoupoteza,  
Ukamrudia yeye Elohimu,  
Hawa alipondanganywa naye Shetani.

**Kwa hali yangu Bwana akanirehemu,  
Akiwa mbinguni,  
Deni yangu akailipa msalabani,  
Ndiye Msamaria mwema,  
Yesu wangu, nitamuishia.**

2. Sheria ya Mungu ilisema nife,  
Kwa dhambi na makosa niliyoridhi,  
Yesu akafa badala ya mimi nife,  
Ili niishi nimsifu milele.
3. Yesu akaniona nikiwa uchi,  
Nafsi yangu akaijaza Roho wake,  
Nangojea mwili wangu ubadilishwe,  
Nijivike vazi langu la utukufu.
4. Ngurumo saba zanena nipokee,  
Nguvu na uweza za Mungu ndani yangu,  
Niwe neno linenalo duniani,  
Na waliolala nao niwaite.
5. Tukutanapo karamuni ya Bwana,  
Huko hewani tumwone Mwokozi,  
Furaha tele huko tutaipata,

Tumwonapo Yesu aliyetukombo.

## **61. A) NI TAMU KUMJUA YESU**

1. Ni tamu kumjua Yesu,  
Na kumwamini pia,  
Kutegemea ahadi,  
Ni sahihi kabisa.

**Yesu, Yesu, namwamini,  
Nikamthibitisha,  
Yesu, Yesu, wa thamani,  
Nizidishwe kumjua.**

2. Ni tamu kumjua Yesu,  
Kumwamini kabisa  
Nizame damuni Mwake,  
Damu ya kutakasa.
3. Ni tamu kumjua Yesu,  
Na kuziacha dhambi,  
Kupokea kwake Yesu,  
Uzima na amani.
4. Ninafuraha kumjua,  
Mwokozi na Rafiki,  
Yeye Yu nami daima,  
Katika maishani.

## **61. B) TIS SO SWEET TO TRUST IN JESUS**

1. Tis so sweet to trust in Jesus,  
Just to take Him at His Word,  
Just to rest upon His promise,  
And to know, "THUS SAITH THE LORD!"

**Jesus, Jesus, how I trust Him!  
How I've proved Him o'er and o'er;  
Jesus, Jesus, precious Jesus!  
Oh, for grace to trust Him more.**

2. Oh, how sweet to trust in Jesus,  
Just to trust His cleansing blood,  
And in simple faith to plunge me,  
"Neath the healing, cleansing flood!"
3. Yes, 'Tis sweet to trust in Jesus',  
Just from sin and self to cease,  
Just from Jesus simply taking,  
Life and rest, and joy and peace.
4. I'm so glad I learned to trust Thee,  
Precious Jesus, Savior, Friend;  
And I know that Thou art with me,



Will be with me to the end.

## **62. UNIUMEGEE MKATE HAI**

1. Uniumegeee Mkate Hai,  
Kama ulivyomega zamani,  
Ninakutafuta, Ewe Bwana,  
Roho yangu yakutaka sana.

**Nitashinda Bwana nitashinda,  
Kama wewe vile ulishinda;  
Nitapita mapitoni mwako,  
Nimeanza Bwana nitashinda.**

2. Uniumegeee Mkate Hai,  
Neno lako likae moyoni;  
Mawazo ya ndani yawe safi,  
Niongozwe daima Mwokozi.
3. Neno lako Bwana, nilione,  
Ujumbe wako niandikie;  
Tushirikiane na upendo,  
Unifinyange kwa sura yako.
4. Muhuri wa saba umevunja,  
Mkate wangu wa uzima,  
Unifanye neno liishilo,  
Nikudhihirishe duniani.
5. Huu Mkate ni ule mwaliko,  
Unaita tai washiriki;  
Imani kweli ya unyakuzi,  
Tukulaki, Eh Yesu angani.

## **63. NINATUMAINI YESU MKOMBOZI WANGU**

1. Ninakutumaini ewe Bwana Yesu,  
Yote yale usemayo wewe unatimiza,  
Ukaniahidi imani ya Baba zetu,  
I ndani ya nafsi yangu nitakuishia.

**Nafsi yangu tulia ndani ya Yesu,  
Ndiye aliye Mkombozi wangu wa ajabu,  
Alinitoa gizani iliyo ya kifo,  
Na kunileta ndani ya nuru ya jioni.**

2. Hawa alipondanganywa naye huyo Shetani,  
Wakaupoteza huo uzima wa milele,  
Kwa Jina lako ukaapa utaukomboa,  
Uzima u ndani yangu, sitaonja kifo.
3. Walipoupoteza uzima wa umilele,  
Pia walipoteza ujana wa umilele,

Lakini Yesu ulilipa deni msalabani,  
Ujana wa umilele sasa urithi wangu.

4. Mihuri saba yote wewe uliivunja,  
Imani ya kunyakuliwa ikafunuliwa,  
Inaimarika ndani ya nafsi yangu,  
Njia ya Elija na Enoko nitapita.
5. Uliniahidi hiyo afya kamilifu,  
Ambapo hakuna magonjwa yatanishika,  
Tena utawala juu ya haya maumbile yote,  
Hata kuita walalao twende nyumbani.

## **64. HAPO KATIKA ENEO LA SABA**

**Nitamuona x2**

**(Huko) eneo la Saba**

**Nitamuona Yesu Mkombozi**

Kumuona	Kumuinua
Nitamuona	Nitamuinua

Kumwabudu	Kumrukia
Nitamwabudu	Nitamrukia

Kumsujudu	Kumchezea
Nitamsujudu	Nitamchezea

Kumsifu	Kumtukuza
Nitamsifu	Nitamtukuza

Anivike	Kumwimbia
Atanivika (Na taji)	Nitamwimbia

Nimvike  
Nitamvika(Na taji)

**Naye atasema**  
**“Ewe mwanangu**  
**Hutalia tena**  
**(sasa) sasa uko nyumbani**  
**Tuishi nawe hata milele”**

x2

## **65. IT'S ALL OVER ME**

It's all over me and it's keeping me alive,  
Keeping me alive, keeping me alive,  
It's all over me and it's keeping me alive,  
Jesus is keeping me alive.

It's Holy Ghost and Fire.  
It's all seven thunders.  
It's all seven virtues.  
It's the Message of the hour.  
It's the Life of Jesus Christ.





It's the love of the Lord.  
It's the blessing of the Word.  
It's the Spirit in my soul.  
It's the promise of the hour.  
It's unfolding of the Word.  
It's the will of the Lord.  
It's the light of the hour.

## **66. UFALME WA JIWE**

1. Nebukadinezari mfalme,  
Aliota ndoto ya ajabu,  
Ya falme nne za mataifa,  
Akafunuliwa na Danieli.

**Na jiwe (hili) ndiye Yesu,  
Kuja nafsini uninyakue,  
Na ufalme wako uuhifadhi,  
Nafsini mwangu.**

2. Hili jiwe likaonekana,  
Likibomoa hizo falme,  
Likawa mlima duniani,  
Na ndio ufalme tutaishi.
3. Muhuri wa saba ulipovunjwa,  
Jiwe hili likaonekana,  
Likishuka humu duniani,  
Ndani ya Bi-arusi wa Yesu.
4. Jiwe hili lindani yake,  
Bi-arusi na amejielewa,  
Ndiye anaufunika mlima,  
Mlima huo wa Sayuni.
5. Bi-arusi anazo ahadi,  
Akamilike kama Yesu,  
Kama wazo tutasafiri,  
Tukutane na Bwana hewani.

## **67. BI-ARUSI AMEKARIBIA KWENDA**

1. Mtu mmoja mikononi mwa Mungu,  
Mara saba duniani kazunguka,  
Sauti iliyo ya mpenzi Bwana,  
(Ikimuita Bibi-Arusi) x2

**Bibi-arusi amekaribia kwenda,  
Amesikia mlio wa Tai,  
Wa Malaki nne Ufunuo kumi,  
(Ule mwaliko Bwana akishuka) x2**

2. Nabii akatuletea ujumbe,  
Ndio mavazi ya Bibi-arusi,  
Una imani ya kutunyakua,

(Tujumuike na Yesu hewani) x2

3. Mihuri saba imefunuliwa,  
Ndicho chakula cha Bibi-arusi,  
Nguzo la Moto ishara ya maajabu,  
(Kuthibitisha ukweli wa Mungu) x2
4. Siri za Mungu zimefunuliwa,  
Kumuandaa Bibi-arusi,  
Nayo maajabu yamesikika,  
(Kote ujumbe umeaminiwa) x2
5. Ndugu na dada hebu jiulize,  
Umefanana na Neno la Mungu,  
Je? Maisha yako kweli yaustahili,  
(Huo ujumbe wa Bibi-arusi?) x2

## **68. BWANA HEBU NIWEPO BI-ARUSI**

### **AIGIAPO**

Bibi-arusi...aingiapo...  
Bi-arusi anapoingia  
Bwana naomba, nami niwepo,  
Kati yao wanaoingia.

Wateule...waingiapo...  
Wateule wanapoingia,  
Bwana naomba, nami niwepo,  
Kati yao wanao ingia.

-Waliojazwa.                      -(Na) wapedwa.  
-(Na) washindi.                 -(Na) wakristo.  
-Walioalikwa.                    -Wenye upendo.  
-Wenye imani.                    -Wabarikiwa.  
-Wanatai.

## **69. UKOMBOZI MKAMILIFU**

Sikufanya lolote kustahili,  
Neema Yake imeniwezesha,  
Kabla msingi wa ulimwengu,  
Nilikuwa niani Mwake.

**Ukombozi mkamilifu,  
Kutokana na dhambi, kizazi kiovu,  
Bwana Mwenyewe ameshuka,  
Neno ni dhahiri, kamwe hatutapotea x2**

We have heard Mother Eagle cry,  
We'll fly above the things of this earth,  
For his Word is made life,  
In us this end time bride.

**We have received our full redemption,**



**From a life of sin, in this evil age,  
The Lord has descended in this day,  
(The Word is made plain, we'll never be lost  
again) x2**

### **70. IN HEAVEN I WILL**

(I'm gonna: \_\_\_\_\_ in heaven one day) x4

-Walk	-Sing
-Shout	-Shine
-Praise	-Jump
-Rest	-Dance

### **71. CHA KUTUMAINI SINA**

1. Cha kutumaini sina,  
Ila damu yake Yesu;  
Sina wema wa kutosha,  
Dhambi zangu kuziosha.

**Kwake Yesu nasimama,  
Ndiye mwamba ni salama;  
Ndiye mwamba ni salama,  
Ndiye mwamba ni salama.**

2. Njia yangu iwe ndefu,  
Yeye hunipa wokovu;  
Mawimbi yakinipiga,  
Nguvu zake ndizo nanga.

3. Damu yake na sadaka,  
Nategemea daima;  
Yote chini yakiisha,  
Mwokozi atanitosha.

4. Nikiitwa hukumuni,  
Moyoni nina amani;  
Nimevikwa haki yake,  
Sina hofu mbele yake.

### **72. JESUS TOOK MY BURDENS**

Jesus took my burdens,  
And rolled them in the sea,  
He rolled them in the sea,  
He rolled them in the sea;  
Now I have the peace,  
That He has given me;  
All my cares and burdens,  
He rolled them in the sea.

-Sins(them)	-Troubles(them)
-Worries(them)	-Blindness(it)
-Sickness(them)	-Sadness(it)

-Fears(them)

-Sorrows(them)

### **73. JESUS IS MINE**

**Jesus is mine x2  
Jesus today is mine;  
I told satan, "get behind me"  
Jesus today is mine.**

-Heaven	Holy Ghost
-Joy	-Peace
-Redemption	-Victory
-Healing	-Divine love
-Faith	-Praising
-Revelation	-Perfection
-Adoption	-Body change
-Rapture	

**Yesu ni wangu (x2)  
Yesu leo ni wangu;  
Kamwambia, "We shetani,  
Rudi nyuma yangu."**

-Ufunuo	-Ukombozi
-Uponyaji	-Ushindi
-Furaha	-Urithi
-Unyakuzi	

### **74. SERVING THE LIVING GOD**

**We are serving the living God x3  
Halleluyah Jesus Christ.**

-Mighty God	-Jehovah Jireh
-Messiah	-Jehovah Shammah
-Who changes not	-Jehovah Nissi
-The conqueror	-Jehovah Tsidkenu
-The living God	-Jehovah Raah
-The Holy God	-Jehovah Rapha
-The King of Kings	-Jehovah Shalom
-The Lord of lords	

### **75. NAKUPENDA BWANA YESU**

Nakupenda Bwana Yesu	} x2
Nakupenda sana	

Nakuinua	Wewe ni Ebeneza
Nakusifu	Wewe ni kimbilio,
Nakuabudu	Wewe ni El-shadai
Nakuenzi	Wewe Yehova-Rapha...

Ufunuo umenipa	Wokovu umenipa
Hekima umenipa	Umenijaza Roho



## 76. A) FURAH KUU ANGANI

Itakuwa x2  
Itakuwa ni furaha tele (tele x2)  
Tumuonapo mpenzi Yesu,  
Aliyetufia msalabani

-Tukinyakuliwa            -Tukimuenzi  
-Tukimwimbia            -Tukimshukuru  
-Tukimwabudu            -Tukimwinua  
-Tukimsujudu            -Tukikaribishwa  
-Tukimwinamia            .....

**Oh! Halleluya x2**  
**Itakuwa ni furaha tele (tele x2)**  
**Tumwonapo mpenzi Yesu,**  
**Aliyetufia msalabani**

## 76. B) GREAT JOY IN THE AIR

What a joy x2  
What a joy there will be in the air (in the air)  
When we see our lover Jesus  
He who died for our sins on the cross.

-After the rapture                            -As we bow to Him  
-As we sing to Him                            -Praising our Saviour  
-As we adore Him  
-Thanking our Saviour  
-As we worship Him  
-As we be welcomed

**Oh! Halleluyah x2**  
**What a joy there will be in the air(in the air)**  
**When we see our lover Jesus**  
**He who died for our sins on the cross.**

## 77. OH LORD, HERE I AM, RIPEN ME

1. We have entered now the harvest time,  
The climax can be seen,  
Of wickedness that is in the world,  
And God's righteousness.

**Oh Lord, here I am,**  
**Laying in the presence of the Son,**  
**Let the rays from the golden cross,**  
**Ripen me.**

} x2

2. It's harvest time, and I must get ripe,  
Lord hear my prayer,  
The stature of a perfect man,  
Lord, that's my cry.

3. The seed has become the seed again,  
The shuck is pulled away,  
The Bride is already golden brown,  
The rapture is at hand.
4. Behold, the Bridegroom cometh,  
To take the ripened Bride,  
We shall only raise up the sleeping Bride,  
And meet Him in the air.

## 78. A) NARUDI NYUMBANI BWANA

1. Naliacha giza kuu kweli,  
Nyumbani naja Bwana,  
Nimeskia mlio wako,  
Nyumbani naja sasa.

**Narudi, narudi,**  
**Kutoka mautini,**  
**Yesu unikaribishe,**  
**Nyumbani naja sasa**

2. Nuru ya jioni umeileta,  
Nyumbani naja Bwana,  
Wafunua jina lako,  
Nyumbani naja sasa.
3. Ulimtuma nabii Elija,  
Nyumbani naja Bwana,  
Imani ya mitume unipe,  
Nyumbani naja sasa.
4. Ngurumo saba sasa zinanena,  
Nyumbani naja Bwana,  
Imani ya unyakuzi unipe,  
Nyumbani naja sasa.
5. Unifanye neno mwilini,  
Nyumbani naja Bwana  
Niwaite wetu walalao,  
Twende nyumbani.

## 78. B) LORD I AM COMING HOME

1. I've left the darkness of this world.  
Now I'm coming home;  
I've heard thy great shout oh my Lord,  
Lord I'm coming home.

**Coming home, coming home,**  
**From the world of death,**  
**Receive me now O Lord Jesus,**  
**Lord I'm coming home.**



2. You've given us the evening light,  
Now I'm coming home;  
You have revealed your mighty name,  
Lord I'm coming home.

3. You sent Elijah to restore,  
Now I'm coming home;  
Restore me to our father's faith,  
Lord I'm coming home.

4. The seven thunders do now speak,  
Now I'm coming home;  
Give me precious rapture faith,  
Lord I'm coming home;

5. Oh Lord let me be the word made flesh,  
Now I'm coming home;  
Then I'll call the sleeping bride,  
So we all come home.

### **79. A MYSTERIOUS CLOUD**

1. May 17, 1963,  
A cloud appeared in life magazine,  
The world did not know just what it meant,  
But to the Bride of Christ it was God unveiled.

**Oh! Halleluyah this is my Redeemer,  
Halleluyah this is my Groom,  
He comes to take me back home,  
Lord Jesus Christ is His mighty Name.**

2. The prophet stood there with a sword in his hand,  
Taking a book from the Saviour's hand,  
To bring redemption to the sons of God,  
And to judge the world for their sins.

3. Now we are waiting for that resurrection day,  
When the dead in Christ shall rise from the grave,  
Then there will be a re-union in the air,  
Of the Bride of Christ and Christ the Lord.

### **80. NEVER GET WEARY YET**

**(I never get weary yet) x2  
I never get weary praising the Lord,  
I never get weary yet.**

(I feel like dancing now) x2  
I feel like dancing praising the Lord,  
I feel like dancing now.

-Waving now -My heart is burning now  
-Shouting now -I feel like traveling on  
-Jumping now -Feel like pressing on

-Clapping now -Am so blessed now  
-Singing now -Feel so happy now  
-I must be moving on.....

### **81. YUBILE YA WAKATI WA MWISHO**

1. Yesu alipokuwa msalabani,  
Alisema yote yamekwisha,  
Deni yote ya dhambi akalipa,  
Yubile ya Bwana nikaipata

**Nimeipata (mimi) nimeipata  
Yubile ya Bwana Mkombozi** } x2

2. Ilipotimu siku ya Pentekoste,  
Mitume wakajazwa na Roho,  
Wakawekwa huru nafsini mwao,  
Yubile ya Bwana wakaipata.

3. Mihuri saba ilipofunuliwa,  
Uhai wa mwana-kondoo nikaupata,  
Umefichwa humu nafsini mwangu,  
Niko huru sasa ndani ya Yesu.

4. Mwili wangu sasa watazamia,  
Kupokea Yubile ya Bwana,  
Nibadilishwe na kwenda angani,  
Nikutane na Yesu Mkombozi.

5. Maumbile yote yatazamia,  
Kudhihirishwa kwa wana wa Mungu,  
Tupeane wokovu kwa wapendwa,  
Tuwaite walalao twende nyumbani.

6. Shetani atachomwa motoni,  
Utawala miaka elfu moja ukiisha,  
Dunia nayo isafishwe na moto,  
Ipate ukombozi wa Yesu

### **82. MUNGU AKINENA KUPITIA BI-ARUSI**

Tukisimama na neno la wakati,  
Itadhihirika sisi tu Bi-arusi,  
Sauti ya Yesu iliyo ndani yetu,  
Itatuwezesha kufanya hayo yote.

-Tukisimama na neno la wakati  
-Tukiwa na moyo mmoja kati yetu  
-Tukimfunga Shetani kama fundo  
-Tukiwa nazo nguvu za uumbaji  
-Tukinenea wenzetu viungo vyao  
-Tukinena wokovu kwa wapendwa  
-Tukitawala maumbile duniani  
-Tukisafiri kama mawazo yetu  
-Tukipitia ukuta kama Yesu



- Tukitembea juu ya maji kama Yesu
- Tukiwaita wetu walalao
- Tukitukuzwa na kwenda angani

(Sauti) sauti ya Yesu iliyo ndani yetu, } x2  
Inatuwezesha kufanya haya yote

### 83. MARA NYINGINE BWANA

1. Samsoni alikuwa mnadhiri wa Bwana;  
Nguvu zake zilifichwa nyweleni mwake,  
Tena alikuwa mwamuzi mkuu wa saba,  
Mungu alijidhihirisha akashinda adui zake.

(Mara nyingine Yesu) x2  
Nipe nguvu zako Bwana nishinde ya dunia;  
Imani ya unyakuzi uiimarisha nafsini,  
Tukutane hewani ewe Mkombozi wangu.

2. Alipofunua siri yote kwa Delila,  
Ya nguvu zake adui wakamng'oa macho,  
Akiwa kipofu aliongozwa na mvulana,  
Kama vile tuliongozwa na madhehebu,
3. Waliandaa karamu awachezee,  
Nywele ilikuwa imekua tena wasijue,  
Akaomba Mungu amrehemu mara nyingine,  
Adui wengi wakafa alipobomoa nyumba.
4. Nabii alidhihirisha Neno na akalala,  
Ndiye aliyekuwa macho yake Bi-arusi,  
Bi-Arusi akaonekana amefifia,  
Bali ngurumo saba zinamkomaza sasa.
5. Bi-arusi wa Omega amesharejeshwa,  
Anazo nguvu na uwezo wa Bwana Yesu,  
Kufinywa kukija sisi tutashinda yote,  
Tuite walalao twende sote nyumbani.

### 84. MUNGU WANGU BABA UMENTIOSHA

Mungu wangu, Baba, umenitosha x2  
Neema yako, Baba, imenitosha x2

- “Kwa kunipea Wewe ni, Jehovah-Jireh” x2
- “Kwa kunichunga Wewe ni, Jehovah-Raah” x2
- “Kwa kuniponya Wewe ni, Jehovah-Rapha” x2
- “Kwa kunikinga Wewe ni, Jehovah-Nissi” x2
- “Kwa amani Wewe ni, Jehovah-Shalom” x2
- “Kwa haki Wewe ni, Jehovah-Tsidikenu” x2
- “Kwa kuwepo Wewe ni, Jehovah-Shammah” x2

Yesu wangu Wewe u haya yote x2  
Naungama, Bwana, umenitosha x2

### 85. MAOMBI YANGU BWANA

1. Naja kitini chako cha rehema,  
Yesu uyasikie maombi yangu,  
Nafsi yangu yakutumaini Bwana,  
Pia we kimbilio shida zijapo.

Nitimizie ahadi zako Bwana,  
Jina lako nizidi kuliinua,  
Nuru ya jioni iangaze nafsini,  
Niwe mkamilifu kama wewe ulivyo.

2. Imani ya Baba zetu uliniahidi,  
Sasa Malaki nne inapotimia,  
Kanisa takatifu lidhihirishwe,  
Lisilo na mawaa wala kunyanzi.
3. Kutimia kwa ufunuo kumi,  
Imani ya unyakuzi imo nafsini,  
Tiisha mwili wangu chini ya Neno,  
Ubadilishwe tukutane hewani
4. Yesu uliniahidi kukamilika,  
Niwe neno linenalo duniani,  
Nipeane wokovu kwa wapendwa,  
Tena viungo vya mwili ni wanenee.
5. Sauti ya Malaika Yule Mkuu,  
Umeificha nafsini mwangu Bwana,  
Iimarisha humu ndani yangu,  
Niwaite walalao twende nyumbani.

### 86. LORD JESUS YOU DESERVE THE GLORY

You deserve the glory,  
And the honor,  
Lord we lift our hands in worship,  
As we praise Your Holy Name. } x2

For you are great,  
You do miracles so great,  
There is no one else like you. } x2

There is no one else like You.

### 87. HOW DEEP THE FATHER'S LOVE

1. How deep the Father's love for us,  
How vast beyond all measure,  
That He should give His only son,  
To make a wretch His treasure.  
How great the pain and searing loss,  
The Father turns His face away,



As wounds which mar the Chosen One,  
Bring many sons to glory.

- Behold the Man upon the cross,  
My sin upon His shoulders,  
Ashamed I hear the mocker's voice,  
Call out among the scoffers.  
It was my sin that held Him there,  
Until it was accomplished,  
His dying breath has brought me life,  
I know that it is finished.
- How great the gulf that God did span,  
To come where I lay helpless,  
Through tears I see His outstretched hand,  
As he declares me guiltless.  
How great the love that sought me out,  
How infinite His mercy,  
His Blood has cleansed my every part,  
And claims me as His purchased.
- I will not boast in anything,  
No gift no power no wisdom,  
But I will boast in Jesus Christ,  
His death and resurrection.  
Why should I gain from His reward?  
I cannot give an answer,  
But this I know with all my heart,  
His wounds have paid my ransom.

## **88. I'VE GOT TO PROVE I'M ONE IN A MILLION**

- It's a challenge to accept,  
It's a faith to rise into,  
It's a way I can show the world  
That Jesus Christ is true;  
It's a life to live, a testimony blameless,  
Living for Christ, standing every test.  
  
**For I've got to prove  
I'm one in a million,  
I've got to show the power of the blood;  
I've got to prove I'm not like those  
from Satan's Eden,  
I've got to show that I'm a person  
that this world isn't worthy off.**
- True representative of Christ,  
In the field that you've been placed,  
The joy of your life with Him,  
Always a glowing on your face;  
Living humbly, following the ways He showed,  
A true witness, of Christ in this day.

- We are the ones that's going to stand,  
And keep a testimony clean  
In the midst of an unbelieving world,  
We'll keep looking to the unseen;  
To really know that we will overcome,  
And receive His promise to sit on His throne.

## **89. WE COME FROM FAR**

We come from far, from far, } x2  
From far to serve the Lord; }  
We come from far, } x2  
We come from far to serve the Lord. }  
  
It's through grace, through grace, } x2  
Through, we serve the Lord; }  
It's through grace, } x2  
It's through grace, we serve the Lord. }

**My tent is no more pitched,  
Down there in Egypt land;  
You'll see me no more there,  
I live in another land.**

Halleluyah, halleluyah,  
Halleluyah, halleluyah.

## **90. HIS NAME IS JESUS CHRIST**

What a King Theophany, that I worship, x3  
King of kings His Name's Jesus Christ.

-Mighty God	-Healer
-Caring God	-Loving God
-Mighty conqueror	-Deliverer
-Redeemer	-Precious God
-Wonderful God	-Creator
-Holy God	-Awesome Father
-Righteous God	-Prince of peace
-Revealed God	-Counselor

.....  
**Halleluyah, Halleluyah  
King of kings His Name's Jesus Christ.**

## **91. UKOMBOZI NA UHAMISHO**

- Muhuri wa saba umefunua ukombozi wangu,  
Damu yake Yesu imeniosha dhambi zangu,  
Dunia inakombolewa Edeni irejeshwe,  
Tuishi naye milele.





**Ninamwabudu Yesu,  
Kwa kunikomboa  
(kwa damu) Kwa damu yake ya thamani,  
(Mimi) Niko huru sasa.**

2. Neno limefunua huyu Melkizedeki,  
Ndiye Yesu Kristo aliye Mwombezi wangu,  
Amenipa uhai wake, nimekombolewa  
Pamoja na urithi wangu.
3. Ukombozi wa Yesu sasa wanihamisha,  
Toka ustaarabuni wa Edeni ya shetani,  
Hadi ustaarabuni huo wa imani,  
Ya dunia”kwaheri.”
4. Ukombozi mkamilifu ni ahadi yangu,  
Natazamia mwili mwangu ulio wa neno,  
Pia mwili wa mavumbi ubadilishwe,  
Tumlaki Yesu hewani.
5. Maumbile yatazamia tudhihirishwe,  
Sisi wana wa Mungu na tuite walalao,  
Wafufuke na miili iliyo ya utukufu,  
Sote tunyakuliwe.

## **92. KUJITAMBUA NA KWENDA UNYAKUZI**

1. Malaika alimwita Gideoni,  
Shujaa akomboe Waisraeli,  
Kutokana na Wamidiani,  
Akaweza alipojijua.  
  
**(Sasa) Sasa niko mbele ya kioo (cha Neno),  
Niwezeshe nijitambue;  
(Namna) Namna Yesu unavyonijua,  
Nikamilike twende nyumbani.**
2. Daudi alizaliwa wa nane,  
Katika nyumba ya Yese,  
Alipotambua yu mfalme,  
Akatawala Israeli.
3. Esteri bi mfalme Ahasuera,  
Alijitambua akaokoa,  
Wayahudi na hila hiyo,  
Ya Hamani wauliwe.
4. Malaika mkuu aliposhuka,  
Malaki nne ilipotimia,  
Anajifunulia Bi-Arusi,  
Twajitambua twende nyumbani.
5. Bwana aliniahidi,

Kuwa neno mwilini,  
Hata imani ya unyakuzi,  
Tukutane hewani.

## **93. BI-ARUSI KATIKA CHUMBA CHA**

### **KUVAA**

1. Kutimia kwa ufunuo kumi,  
Huyu Malaika mkuu akashuka,  
Na baraka za Bi-arusi,  
Twazipokea tufanane naye.  
  
**(Yesu) Yesu nivike na kimo,  
Cha mtu mkamilifu;  
(Mimi) Duniani nikudhihirishe,  
Jina lako takatifu litukuzwe.**
2. Nimesimama mbele ya Kristo,  
Neno la wakati alifunua,  
Ili nichukue sura yake,  
Nibadilishwe, nifanane naye.
3. Nimepokea Roho wa Kristo,  
Nia yake imo ndani yangu,  
Nimefanyika mateka wake,  
Ananiongoza maishani.
4. Nimevaa silaha za vita,  
Ni Neno lililofunuliwa,  
Ili nipigane na shetani,  
Bwana anishindania vita.
5. Upendo wa Mungu u ndani yangu,  
Ili nitawale hali zote,  
Sauti ya Malaika mkuu,  
Inaimarika niite walalao.
6. Siri ya kuja kwake amenipa,  
Nguo nyeupe imo nafisini,  
Tena imani ya unyakuzi,  
Nitukuzwe niende karamuni.

## **94. WIMBO WA HARUSI**

1. Sisi tumekuja hapa siku ya leo,  
Kushuhudia Neno lake Mungu,  
Nyinyi maharusi kwamba mmewaacha,  
Wazazi wenu ili muwe mmoja.  
  
**(Ahsante) x2 Bwana Yesu,  
Umeshindania hawa (vita);  
Vita iliyo kuu duniani,  
Wavike na upendo wako.**



2. Siri ya kuoja sasa imefunuliwa,  
Mlikuwa mawazoni mwake Elohim,  
Mmedhihirishwa humu duniani,  
Kama Yesu Kristo na Bi-Arusi.
3. Ni kitu kizuri Yesu amekupa,  
Yeye ni nyama ya nyama zako ndugu,  
Hata mifupa na roho zako pia,  
Umpende namna ujifanyavyo.
4. We're promised greater works  
Beyond the early church  
We'll also preach to the lost ones  
And express Christ's great glory
5. With the creative power  
We will pull the sleeping Saints  
Then have a body change  
And meet Jesus in the skies

**Bridge**

**Oh Lord Jesus  
Let me recognize myself  
And be restored to my Sonship**

**Then show your power  
Before going back home**

**123. A) JIBU LA BI-ARUSI KWA MWOVU  
SHETANI**

1. Israeli katika vitani na wafilisti  
Goliathi alitukana Mungu wa Israeli  
Tena kuuliza nani angepigana naye  
Daudi kwa jiwe moja la matano akamuua  
  
**Yesu nizamishe zaidi ndani ya Neno Lako  
Nifanyike Neno linenalo duniani  
Niwe jibu kwa swali la mwovu shetani  
Nitwae ushindi wangu wakati huu wa mwisho.**
2. Eliya na manabii hao wa Baali  
Wakakutana mlimani mwa Karmeli  
Ijulikane Mungu gani ndiye wa kweli  
Yehova alijidhihirisha kwa utukufu mwingi
3. Yesu aliteswa na kuangikwa msalabani  
Shetani akahasabu amemshinda Bwana  
Mkombozi akasema yote yamekwisha  
Akatulipia deni yote ya dhambi
4. Kwa Mwanakondoo kuvunja Muhuri wa Saba  
Twapokea uhai wake nafsini mwetu  
Na kushiriki tabia yake Mungu  
Tudhihirishe Mwana wa Adamu maishani haya
5. Tumepokea ahadi ya upendo mkamilifu  
Twatawala hali zote duniani  
Pia kumfunga Shetani kama fundo  
Sote tubadilishwe tumlaki Yesu hewani

**123. B) THE BRIDE'S ANSWER TO THE  
DEVIL**

1. As Israel fought with Philistines  
Goliath cursed the God of Israel  
And dared an Israelite to fight them  
David with a slingshot and stone killed him  
  
**Jesus take me deeper in your Word  
Let me be the Word made flesh on earth  
I be the answer to the devil's question  
And possess my victory in these last days**
2. Elijah and the prophets of Baal  
Met on Mount Carmel for showdown  
To prove who the true God was  
Jehovah manifested Himself with great glory





3. Jesus was afflicted and put on the cross  
Satan thought he had defeated the Lord  
The redeemer proclaimed that all is finished  
Thus paid all the debt of our sins
4. The Lamb of God broke the 7<sup>th</sup> seal  
We are receiving His Literal Life  
Being made partakers of Divine Nature  
To manifest the Son of Man in our lives
5. We have received the promise of Divine Love  
To master every situation  
Also bind Satan like a knot  
Then all be changed and meet Jesus in the air

#### **124. A) KUJENGA TENA HEKALU HAI WAKATI HUU**

1. Wayahudi walihamishiwa Babeli  
Walipotekwa na Nebukadnezari  
Kwa hatua tatu walipelekwa  
Ndivyo kanisa lilianguka toka Neno  
  
**Mkombozi wangu Yesu nirejeshe  
Kikamilifu kwa imani ya Baba zetu  
Malaki nne yaniweka nuruni (Mwako)  
Nibadilishwe ninyakuliwe**
2. Kanisa lilizaliwa Pentekoste  
Yesu akawa hai miongoni mwao  
Unikolai, ubalamu na uyezebeli  
Zikaangusha kanisa la Alfa
3. Baada ya miaka sabini  
Mfano wa nyakati za kanisa  
Babeli ikaanguka, Yuda wakarudi  
Nasi tumetoka Babeli ya siri
4. Walirudi Yuda kwa hatua tatu  
Baadaye wakaimarika nchini mwao  
Twahesabiwa haki na kutakaswa  
Twajazwa Roho kisha kukamilika
5. Mfalme wa Uwajemi aliagiza  
Hekalu la Mungu lijengwe tena  
Vifaa vya ujenzi walitoa mlimani  
Urejesho wetu watoka Mlima Machweo
6. Kitabu cha sheria kililetwa  
Wakafunzwa na watumishi wa Mungu  
Neno tumerejeshwa, nao Utukufu  
Wa Kanisa la Omega uzidi wa Alfa

#### **124. B) REBUILDING OF THE LIVING TEMPLE IN THIS TIME**

1. The Jews were taken to captivity  
In Babylon by Nebuchadnezzar  
They were carried away in three stages  
Like the true church fell from the Word  
  
**Jesus my redeemer, restore me perfectly  
To the faith of our fathers  
Malachi 4:5 brings me into your Light  
For my change and translation**
2. The church was born at Pentecost  
Jesus was alive among them  
Nicolaitanism, Baalamism and  
Jezebelism made the Alpha church fail
3. After the 70 years passed  
Same as the 7 church ages  
They returned home after Babylon fell  
We have come out of mystery Babylon
4. They returned to Judah in three stages  
As the true church of God goes on  
We get justified, sanctified by the blood  
Then Holy Ghost baptism unto perfection
5. The king of Persia gave the order  
Of the rebuilding of the temple of God  
The materials came from the mountain  
Our restoration comes from Mt.Sunset
6. After the book of law was brought  
The servants of God taught them  
We have received the restored Word  
Omega church will exceed Alpha in glory

#### **125. A) UREJESHO NA KUKOMAA KWA BI- ARUSI**

1. Kanisa la Yesu lilizaliwa  
Pentekoste walipojazwa  
Roho Mtakatifu nafsini  
Kanisa kamilifu likadhihirishwa  
  
**E Bwana Yesu hebu nikae  
Juani mwako unyevu uishe  
Kwa Malaki nne kutimia natwaa  
Kimo cha mtu mkamilifu**
2. Maumbile hufunua mpango wa Mungu  
Mbegu ya ngano inapopandwa  
Hukua hadi kutoa mazao





Punje nyingi kama ya asili

3. Kanisa la Alfa lilikuwa punje  
Kisha likazikwa chini ya dini  
Neno la Mungu lilipochanganywa  
Na uongo, giza likaingia dunia
4. Kumea kwa ngano kukaja na Luther  
Kuhesabiwa haki, Wesley  
Akaleta kishada cha utakaso  
Kapi ya kipentekoste, vipawa
5. Uhai wakusanywa kwenye mbegu  
Punje yakomaa na kuacha kapi  
Nabii alikuwa mganda wa kwanza  
Sasa kanisa la Omega sawa na Alfa
6. Tuna utawala juu ya maumbile  
Tuite wale wetu walalao  
Ngano iwekwe galani kwa unyakuo  
Nayo kapi ifungwe ichomwe

## **125. B) RESTORATION AND MATURITY OF THE BRIDE**

1. The Church of Jesus Christ was born  
At Pentecost when the disciples  
Got filled with the Holy Ghost  
A perfect church was manifested

**Oh Lord Jesus, let me stay  
In thy Sun to ripen  
Fulfillment of Malachi 4 gives me  
The stature of a perfect man**

2. Nature reveals the plan of God  
A grain of wheat is planted  
And grows through to maturity  
Bringing many similar grains
3. The Alpha Church was original grain  
It was later buried under Roman soil  
When the Word was mixed with the lie  
And darkness struck the earth
4. Sprouting of wheat blade was Luther's  
Justification message, the the tassel  
Was Wesleyan sanctification by blood  
And Pentecostals shuck restored the gifts
5. Life is now gathered in the grain  
Seed ripens and separates from the shuck  
The prophet was the first mature sheaf  
Omega church is now same as Alpha

6. We have dominion over the creation  
We shall call the sleeping saints  
The seed is garnered in the Rapture  
And the shuck will be burnt

## **126. A) WEKA ISHARA KWA JAMAA YAKO**

1. Israeli waliua mwanakondoo Misri,  
Na kupaka damu milangoni,  
Walipoonyesha ishara ya damu,  
Wazaliwa wa kwanza wakaepuka kifo.

**Tuwekeni hiyo Ishara,  
Na kuwaingiza wapendwa wetu,  
Tuwekeni hiyo Ishara,  
Maana wakati umeenda sana.**

2. Hukumu ilipoelekea Yeriko,  
Rahabu akafunga hiyo kamba nyekundu,  
Dirishani mwa nyumba yake,  
Na kuokoka pamoja na jamaa yao.
3. Petro alitangaza siku ya Pentekoste,  
Kuwa Ishara hii iliyo Roho,  
Ni yetu na watoto wetu,  
Kwa wote atakaoita Yesu.
4. Tuko wakati wa jioni sasa,  
Weka Ishara kwa wapendwa wako,  
Kupitia imani iliyokuokoa,  
Ikakufanya mmoja na Neno.
5. Mwishoni Yesu atakaporejea,  
Familia ya mbinguni na duniani itaungana,  
Na wakionyesha hiyo Ishara,  
Nasi tutaonyesha Ujumbe wa Tai.

## **126. B) APPLY THE TOKEN TO YOUR FAMILY**

1. Israel killed the lamb in Egypt,  
And applied the blood on the door posts,  
When the token was on display,  
The firstborns in the house were spared.

**Let's apply the Token,  
And bring our families in,  
Let's apply the Token,  
For the hour is late.**

2. When Judgement hang over Jericho  
Rahab hang that scarlet thread,  
On the window of her house,



She was saved with her family.

3. Peter declared at Pentecost,  
That this Token, the Holy Ghost,  
Belongs to us and our families,  
As long as Christ keeps calling.
4. We are now in the evening time,  
Apply the Token to your family,  
With the faith that called you in,  
And made you one with the Word.
5. In the end when Jesus returns,  
The family in heaven and earth unites,  
And as they display their Token,  
The eagle Message, we shall display.

### **127. A) KUAMKA KWA ESTA**

1. Mfalme Ahasuero alipoandaa karamu,  
Vashiti alipuuza karamu hiyo,  
Mfalme akamtaliki na kutwaa Esta,  
Yesu ametema Laodikia na kutwaa Bi-Arusi.

**E Bwana Yesu niko mbele yako,  
Nijitambue nivae sura yako,  
Nidhihirishe ushindi gizani,  
Nibadilishwe tukutane hewani.**

2. Hamani alipanga kuua Wayahudi,  
Namna shetani amepangia Bi-Arusi,  
Mordecai akafichua njama hiyo,  
Bi-Arusi naye atambua hila ya Adui.
3. Mordekai alitumana mara mbili,  
Kamwambia Esta kusudi lake,  
Esta hatimaye akapata kufahamu,  
Akaanza kuomba apate kibali.
4. Mordekai yu mfano wa nabii,  
Neno latoka kwake hadi kwa Hathaki,  
Aliye mfano wa huduma tano,  
Kuamsha Esta Bi-Arusi ajitambue.
5. Esta alijivika mavazi ya kifalme,  
Akapata kibali kwa mfalme,  
Bi-Arusi aliyezaliwa akubalika,  
Yu mrithi pamoja na Yesu.
6. Esta aliokoa hao Wayahudi,  
Hamani na wanawe wakauliwa,  
Nasi twaokolewa toka mautini,  
Kisha shetani atupwe motoni.

### **127. B) AWAKENING OF ESTHER**

1. When King Ahasuerus made a feast,  
His wife Vashti defied his call,  
He divorced her and married Esther,  
Jesus has divorced Laodicia and married the Bride.

**Oh Lord Jesus am before you,  
Help me know myself and be like you,  
To manifest you in this dark world,  
Then be changed to meet you in the air.**

2. Haman planned to kill all the Jews,  
Just as Satan means for the Bride,  
Mordecai exposed the evil plan,  
And the Bride can see the enemy's move.
3. Mordecai sent Hatach 2 times,  
To show Esther the value of her position,  
Esther did finally wake up,  
And began praying for acceptance,
4. Mordecai typed our prophet,  
With a message that comes from Hatach,  
Who types the 5-fold ministry,  
To awaken Esther the Bride.
5. Esther wore the royal garments,  
And found favour with the king,  
The Bride has favour with God,  
And is co-heir with Jesus Christ the Lord.
6. The queen saved all the Jews,  
Haman and his sons were all killed,  
We are saved from death to life,  
While Satan will be cast into the fire.

### **128. A) MWANAMKE MSHUNAMI MFANO WA KANISA LA ALFA NA OMEGA**

1. Mshunami aliandalia Elisha chumba,  
Nabii apate pa kupumzikia kila apitapo,  
Huyo mwanamke akajaliwa mtoto kwa hilo,  
Twabarikiwa kwa kumpokea Yesu nafsinii.

**Yesu nirejeshee haki zangu,  
Hiyo imani ya baba zetu mitume  
Kwa Malaki nne tano kutimia,  
Hebu niwe kanisani tukufu la Omega**

2. Mwana pekee wa mshunami alipokufa,  
Elisha aliomba na mwana kafufuka,  
Naye Yesu Mwana wa Mungu kafa  
Msalabani, bali Mungu akamfufua



3. Elisha kamwambia mwanamke aende ugenini,  
Maana Mungu aleta njaa Israeli miaka saba,  
Mfano wa shida za nyakati za kanisa,  
Mwanamke akaenda pamoja na mwanawe.
4. Miaka saba ilipoisha akarudi Israeli,  
Akiwa na mwanawe akitaka mali yake,  
Kanisa linarudi baada ya nyakati saba,  
Liwe na utukufu wa Omega wa Kimitume.
5. Huyu mwanamke alimlilia mfalme,  
Arejeshewe shamba na mazao yake mengi,  
Mfalme alituma afisa ili amrejeshee,  
Mfano wa Roho akiturejesha kwa huduma tano.
6. Huyu mshunami ni mfano wa kanisa la Alfa,  
Lililoanguka na kuingia gizani nyakati saba,  
Tena la Omega likirejeshwa na utukufu,  
Giza la Laodikia halimo ndani yake.

### **128. B) THE SHUNAMITE WOMAN A TYPE OF ALPHA AND OMEGA CHURCH**

1. The Shunammite woman made Elisha a chamber,  
Where he could rest on his journeys,  
She was childless and got a son for this  
We are blessed for letting Jesus into our souls.

**Jesus restore to me my rights,  
The faith of our Apostolic fathers,  
Now that Malachi 4:5 is fulfilled,  
Let me be in the glorious Omega church.**

2. When the sole son of the Shunammite died,  
Elisha prayed and restored him to life,  
Jesus the son of God died on the cross,  
But the Father raised him from the dead.
3. Elisha told the woman to leave Israel,  
For famine would be in the land 7 years,  
She took her risen son and went away,  
A type of troubles of the 7 church ages.
4. The woman returned with her son to Israel,  
To seek her estate after 7 years,  
And today after 7 church ages,  
The Omega Apostolic church is expressed.
5. The woman went right to the King,  
To ask for her estate and its increase,  
And the king appointed her a restoring officer,

The Spirit used 5 offices to restore us.

6. This woman types the Alpha Church that fell,  
And went through darkness in the church ages,  
Then she types the restored Omega Bride,  
Where the darkness of Laodicea is absent.

### **129. A) UDHIHIRISHO WA MBEGU ZA KIROHO ZA MUNGU**

1. Mungu aliweka sheria ya mbegu,  
Hapo kitabuni cha Mwanzo,  
Kila mbegu ize kwa jinsi yake,  
Nasi tu mbegu za kiroho za Baba.

**Nafsi yangu si ya ukoo wa duniani,  
Mimi ni mbegu ya Mungu Baba,  
Asili Yake imeandikwa nafsini,  
Namdhihirisha kizazi hiki.**

2. Kabla tu ya Mihuri nabii akafunza,  
Kimo cha mtu mkamilifu,  
Chetu kutwaa Mihuri ikivunjwa,  
Tuwe maskani ya Mungu duniani.
3. Jua la haki limetuzukia,  
Roho wa Mungu atuhuisha,  
Ili tuoneshe tabia ya Kiungu,  
Ule upinde wa sifa saba za Bwana
4. Majaribu tofauti yatujiapo,  
Yaimarisha uungu ndani yetu,  
Uliofichwa kwenye nafsi,  
Tuweze kuonesha sura Yake Mungu.
5. Malaika Mkuu Yuko duniani,  
Na kupitia huduma tano halisi,  
Ahuisha Neno ndipo tukomae,  
Tujifahamu vile tunavyofahamika.

### **129. B) THE EXPRESSION OF GOD'S SPIRITUAL GENES**

1. There's a seed law in nature,  
Set by God in Genesis,  
That every seed bring forth its kind,  
And our souls are genes of God.

**My soul is not of earthly parents,  
Am an attribute of God,  
His nature is written within,  
And I will express Him this day.**

2. Before the Seals the prophet taught,



The stature of a perfect man,  
Attainable after Seals open  
God's Tabernacle today

3. When the Son of Righteousness arises,  
The Holy Spirit quickens us,  
The Divine Nature is expressed,  
The rainbow, 7 virtues of God.
4. When divers trials come our way,  
They are to refine God's nature,  
That is hid inside our souls,  
To express the image of God.
5. The Mighty Angel is on earth,  
Working thru a true 5 fold ministry,  
Giving more sense to the Word,  
To make us known as we are known

### **130. A) BI-ARUSI APELELEZA AHADI YA WAKATI**

1. Kwa kufunuliwa kwa hiyo mihuri saba,  
Kanisa lavuka Yordani ya leo,  
Urithi wangu wote unafunuliwa,  
Niwe na kimo cha mtu mkamilifu  
  
**Yesu alinifia Kalvari,  
Kanilipia deni yote ya dhambi,  
Muhuri wa saba umefunua urithi wangu,  
Nami napeleleza kilichomo.**
2. Upendo wa kiungu ni urithi wangu,  
Wadhibiti hali yoyote ikiibuka,  
Nabii akiwa nao alimnenea,  
Dume muuaji na kumtuliza.
3. Nafanyika neno linenalo duniani,  
Kama nabii wa Malaki nne tano,  
Aliyemfufua huyo samaki mdogo,  
Tena akaumba wale kindi kwa kunena.
4. Nabii pia alikemea dhoruba ikatawanyika,  
Akiwa mwana wa Mungu aliyedhihirishwa,  
Wa kwanza kufika ukomavu kwa wakati huu,  
Twayapata haya mamlaka.
5. Eliya alisafiri kwa nguvu za Roho,  
Naye Filipo akainuliwa na Roho,  
Hadi Azoto utumishini mwa Mungu,  
Hii pia ni ahadi yetu wakati huu.
6. Kwa kufunuliwa kwa muhuri wa saba,  
Napokea imani ya unyakuo,

Mwili wangu ubadilishwe chini ya baragumu,  
Ninyakuliwe kukutana na Yesu.

### **130. B) THE BRIDE SEEKING THE PROMISE OF THE HOUR**

1. By the opening of the Seven Seals,  
The Church of Jesus Christ crosses the Jordan today,  
My inheritance is now revealed,  
To give me the stature of a perfect man.  
  
**Jesus died for me at Calvary,  
And paid the price for my sin,  
The 7th seal reveals my possession,  
Am searching it for all that is available.**
2. Divine Love is my portion,  
To master any challenge that comes on the way,  
Thru it the prophet spoke to the killer bull,  
And caused the charging animal to calm.
3. I am becoming the word in flesh,  
Like the prophet of Malachi 4:5,  
Who raised the little dead fish,  
And created seven squirrels by speaking.
4. The prophet also rebuked the storm,  
As a placed, manifested son of God,  
The first one to mature in this age,  
We are getting the same authority to rule.
5. Elijah travelled by the power of the Spirit,  
And Philip was flown by the Spirit to Azotus,  
While they were in the Lord's service,  
This too is the portion of the Bride today.
6. The opening of the 7<sup>th</sup> Seal,  
I am receiving Rapturing faith,  
My Body will be changed under the Trump,  
I will rise to meet Jesus in the Rapture.

### **131. A) KUTOKA LAODIKIA HADI IMANI YA UNYAKUO**

1. Huyu Henoko mtu wa saba  
Toka Adamu yule wa kwanza  
Baada ya ushuhuda wa imani  
Kwa muda wa miaka mia tatu  
Ulimnyakua asionje kifo  
  
**Hata leo ndivyo unafanya  
Kwa kuwa Ngurumo saba zanena  
Zatutoa Laodikia ya kifo  
Na kutupa imani ya Unyakuo**



## **Pasipo kifo tupae nyumbani**

2. Eliya naye huyo Mtishibi  
Alionesha Mungu yule wa kweli  
Na akapigana na miungu wa baali  
Akamaliza kazi akavuka Yordani  
Ukamnyakua asione kifo.
3. Bwana Yesu alipomaliza kazi  
Na akasema yote yamekwisha  
Ulimfufua na Utukufu mwingi  
Kwa wingu akapaa na Utukufu mwingi  
Pamoja nao watakatifu wa kale.
4. Kuna kazi We wafanya leo  
Wengi wapashwa hawasadiki  
Ni kazi fupi iliyo ya upesi  
Ya kuandaa Bi-Arusi Wako  
Umtwae asione mauti.
5. Roho Mtakatifu ndani mwetu  
Umetupa akiwa malimbuko  
Ishara ya kuwa urithi wote ni wetu  
Miili yetu nayo itabadilishwa  
Tunyakuliwe pasipo mauti.

## **131. B) FROM LAODICEA TO RAPTURING FAITH**

1. Enoch who was the 7<sup>th</sup> man  
From Adam the first man on earth  
Had a testimony pleasing God  
For a period of 300 years,  
You took him and he never had to die.

**You are doing the same even today  
For the 7 Thunders are speaking  
To take us from Laodicean death  
And give us that Rapturing faith  
So we go home not having to die.**

2. Elijah the prophet from Tishbe,  
Proved that Jehovah is the true God.  
He fought the false gods of Baal  
Finished his work and crossed Jordan,  
You took him and he never did die.
3. After the Lord Jesus finished his work,  
And said that all is now finished,  
You resurrected him with great Glory,  
And a cloud of Glory took Him away  
Together with Old Testament Saints.

4. There is a work that you're doing today  
And many disbelieve though they be told  
It is a quick and very short work,  
To prepare your beloved Bride,  
To make her escape death and go home
5. The Holy Ghost in our hearts  
Is the earnest of full redemption  
To prove the full inheritance is ours  
Showing us our bodies will be changed  
So we translate without tasting death.

## **132. A) BI-ARUSI AKIWA NA VAZI LA ELIYA NA NGUVU ZA MUNGU**

1. Eliya alimdhahirisha Mungu kikamilifu,  
Elisha mtumishi wake alijifunza kwaye,  
Eliya alipopaa hapo Yordani kaacha vazi,  
Elisha akaitwaa pamoja na nguvu za Roho.

**Huduma ya Kristo iliyokuwa na Eliya  
Imemrejea Bi-Arusi wa Kristo  
Tukiwa na vazi la Eliya na Roho wa Mungu  
Tunayo huduma kuu kisha tunyakuliwe.**

2. Musa aliongoza Israeli katika Kutoka,  
Yoshua akajifunza chini ya Musa,  
Musa alipoondolewa, Yoshua katwaa hatamu,  
Na kuongoza Israeli urithini.
3. Yesu alilipa deni ya dhambi Kalvari,  
Na kujaza wanafunzi na Roho Pentekoste,  
Wakaiendeleza huduma ya Bwana Yesu,  
Ishara na maajabu zikaandamana nao.
4. Nabii wa Malaki nne alitumwa magharibi,  
Akakutana na hao Malaika Saba,  
Na kupokezwa ufunuo wa Mihuri Saba,  
Imani ya unyakuo ikafunuliwa papo.
5. Malaika wa Bwana amerejea Bi-Arusi,  
Na kummpa ufunuo wa Kitabu cha urithi,  
Bi-Arusi afanyika sauti ya Mungu duniani,  
Amaliza huduma ya Mwana wa Adamu.

## **132. B) THE BRIDE WITH THE ROBE OF ELIJAH AND POWER OF GOD**

1. Elijah manifested God perfectly,  
Elisha his servant learnt from him,  
Elijah went up at Jordan and dropped the robe,  
Elisha took it and received power for ministry.





**The ministry of Christ that Elijah had,  
Has returned to the Bride of Christ,  
With the Robe of Elijah and Power of God,  
We have a great ministry before the Rapture.**

2. Moses led the Israelites in the Exodus,  
And Joshua learnt from the man of God,  
When God took Moses, Joshua took over,  
And led Israel into their inheritance.
3. Jesus paid our debt at Calvary,  
And the Spirit filled the disciples at Pentecost,  
They continued the ministry of Christ,  
With signs, wonders and miracles following.
4. The prophet of Malachi 4 went west,  
And out there met those 7 Angels,  
He received the Revelation of the 7 seals,  
From there, Rapturing faith came to us.
5. The Angel of the Lord returns to the Bride,  
To give her the Revelation of the Book,  
The Bride becomes the voice of God on earth,  
To finish the Ministry of the Son of Man.

### **133. A) WIMBO WA SHEREHE YA HARUSI**

1. Mungu alimfanyia Adamu Hawa,  
Mfupa kutoka kwa mifupa yake,  
Pia nyama na roho kutoka kwake,  
Ninyi wawili mu kitu kimoja.

**Ndugu....x2**

**Mungu amekufunulia kipawa cha ajabu,  
Mke mwema aliyetoka ndani yako,  
Mwaonyesha Kristo na Mke wake.**

**Dada...x2**

**Mungu amekufunulia kichwa chako,  
Bwana yako uliyetoka ndani yake,  
Mwaonyesha Kristo na Mke wake.**

2. Ilikuwa majira ya jioni,  
Isaka kapatana na mpenzi Rebeka,  
Baada ya Ibrahimu kumtuma Eliezeri,  
Jioni ya nyakati Mungu amekupa mke.
3. Ruthu aliingia shamba la Boazi,  
Kama mfanyikazi na Boazi kampenda,  
Ruthu akawa mrithi pamoja naye,  
Mali yako ndugu sasa mwarithi na mkeo.
4. Yesu alimfia mke wake Kalvari,  
Akamlipia deni yake ya dhambi,

Amezaliwa na Roho wake Kristo,  
Twaelekea Karamu ya Bwana hewani.

5. Japo wakati uliwatenganisha kwa muda,  
Mungu amewaleta pamoja tena,  
Hebu Ngurumo Saba ziwanenee,  
Mkamilike ili kumlaki Yesu hewani.

### **133. B) WEDDING CEREMONY SONG**

1. God made Eve for Adam,  
A bone taken from his bones,  
As well as flesh and Spirit from him,  
You too are the same unit.

**Brother...x2**

**God has revealed to you a precious gift,  
A good wife who came out of you,  
You both manifest Christ and His Wife.**

**Sister...x2**

**God has revealed to you your head,  
The husband whom you came out of,  
You both manifest Christ and His Wife.**

2. It was in the evening time,  
When Isaac met sweet Rebekah,  
After Abraham had sent Eliezer,  
This evening hour, you get your sweet heart.
3. Ruth entered the field of Boaz,  
As she labored Boaz loved her,  
She then became joint heir with him,  
And your wife is a joint heir of your estate.
4. Jesus died for his wife at Calvary,  
And paid the price of her sins,  
She is born of His Holy Spirit,  
Soon we go to the wedding feast on high.
5. Though on earth you were apart for a while,  
God has brought you together,  
May the 7 Thunders speak to you,  
Unto perfection for the Rapture.

### **134. A) HAZINA YA BETHLEHEMU**

1. Salmon, mtawala mmoja huko Yuda,  
Alimwoa Rahabu wa Mataifa,  
Wakaanzisha Bethlehemu, mji wa Daudi,  
Sawa na Kristo na Bi-Arusi Wake.





**Kuna Hazina iliyowekwa Bethlehemu,  
Nyumba ya Mkate wa Mungu,  
Ni Ufunuo wa ile Mihuri Saba,  
Hapo tai wakusanyika kwa karamu.**

2. Shamba lilijaa shairi na ngano,  
Alizopanda Boazi, mkombozi wa Ruthu,  
Naye Kristo Mkombozi wetu,  
Ameandaa Chakula cha sehemu Saba.
3. Daudi alitamani maji ya Bethlehemu,  
Askari wake wa Mataifa wakamletea,  
Nasi Bi-Arusi wa Mataifa leo hii,  
Twashinda kwa Upanga wa Mfalme.
4. Yesu alizaliwa huko Bethlehemu,  
Na wachungaji wakamkaribisha,  
Bwana ametutumia wachungaji,  
Sisi tulio wanakondoo wake siku hii.
5. Kristo ameshuka na Mwaliko,  
Mkate toka Mbinguni wa Bi-Arusi,  
Roho Mtakatifu ameachiwa,  
Aliye Nguvu za Unyakuo.

### **134. B) BETHLEHEM'S TREASURE**

1. Salmon, a prince in Judah,  
Married Rahab a Gentile woman,  
They founded Bethlehem, David's city.  
Just like Jesus and His Gentile Bride.

**There is a Treasure set in Bethlehem,  
The House of God's Bread,  
It's the Revelation of the Seven Seals,  
There the eagles gather for a feast.**

2. The field was full of wheat and barley,  
Which Boaz, Ruth's kinsman sowed,  
And Christ our Redeemer has set,  
For us a Seven Seals course menu.
3. David desired the waters of its wells,  
The Gentile warriors fetched it for him,  
And we the Gentile Bride this day,  
With the Sword of the King fight the good fight.
4. Jesus was born in Bethlehem,  
Where shepherds welcomed Him,  
The Lord has sent His shepherds,  
To His lambs in this hour.
5. Christ has descended with a Shout,  
Bread sent from Heaven for the Bride,

The Holy Spirit has been set loose,  
The Dynamics for the Rapture.

### **135. A) AMANI KWAKO BI-ARUSI**

1. Nchi ilikuwa ukiwa na utupu,  
Mungu akasema, "Na iwe nuru".  
Ikawa Edeni ya kupendeza,  
Afanya hilo nasi sasa.
- Amani Bi-arusi Mpendwa,  
Amani Wateule wa dhamani,  
Siku ya nane yapambazuka,  
Nyota ya asubuhi yazuka mioyoni**
2. Yesu alipofufuka toka wafuni,  
Baada ya kushinda nguvu za dhambi,  
Aliwatokea wanafunzi akisema,  
"Amani na iwe kwenu".
3. Baada ya giza la madhehebu,  
Mungu alivunja Mihuri na kushuka,  
Sasa tu wakatini wa Bi-arusi,  
Twakusanywa ili tunyakuliwe.
4. Je, umekutana na Malaika usiku,  
Kashindana Naye hadi asubuhi?  
Jina lako litabadilishwa,  
Utembee na Mwana aliyechomoza.

5. Ni kuzuka kwa siku mpya,  
Kilio chawepo usiku tu,  
Bali furaha yaja asubuhi,  
Amani! Ni kuchomoza kwa Mwana

### **Daraja**

**Leo ni siku Bwana aliofanya,  
Jiwe la Kilele mwishowe li hapa,  
Kazi ya ajabu machoni petu,  
Tutafurahia sikuni hii.**

### **135. B) SHALOM UNTO YOU BRIDE**

1. The earth was dark and void,  
But God said "Let there be light."  
Transforming it to a beautiful Eden,  
As He's doing in our lives.

**Shalom Beloved Bride,  
Shalom Precious elect,  
It's the dawning of the 8th day,  
The day Star is arising in our hearts.**

2. When Jesus Christ rose from the dead,



Having loosed the grip of sin,  
He appeared unto them saying,  
“Peace be unto you.”

3. After denominational ages,  
God came down and broke the seals,  
We're now in the Bride age,  
Being gathered for the Rapture.
4. Have you met the Angel at night,  
And wrestled with Him till dawn?  
Your name will be changed,  
And limp with the risen Son.
5. It's the breaking of a new day,  
Weeping may endure only for a night,  
But joy comes in the morning,  
Shalom! It's the rising of the Son.

### Bridge

**This is the day God has made,  
The rejected Capstone has come,  
The Lord's doing that's marvelous,  
We will rejoice and be glad in it.**

### 136. A) MIKAYA SHAHIDI WA KWELI

1. Kulikuwa na amani Israeli,  
Baada ya vita viwili na Shamu,  
Twasimama siku ya leo,  
Baina ya vita vya pili na tatu.
- Mmoja kama Mikaya yu hapa,  
Akishikilia Ujumbe wa Eliya,  
Mimi ni mmoja kama Mikaya,  
Shahidi wa kweli wa Kristo.**
2. Alikuwapo nabii katika nchi,  
Naye alifunguliwa macho,  
Aweze kuona unabii wa siku ile,  
Mikaya mfano wa Bi-arusi.
3. Mjumbe wa Ahabu kawa na hila,  
Bali Mikaya akaungama kuwa,  
Nitasema tu aliyosema Mungu,  
Shahidi mwaminifu wa Mungu.
4. Bi-arusi afanya nia ya Mungu,  
Halazimishwi kufanya lingine  
Ana "Hivi asema Bwana",  
La sivyo anyamaza kabisa.
5. Mikaya kaona pepo mwongo,

Akiwapaka manabii wa Ahabu,  
Kama vyura wa Ufunuo kumi na sita,  
Kuongoza wafalme Har-magedoni

6. Roho wa Eliya yu hapa,  
Kumpaka Bi-arusi siku hii,  
Kumfunulia ule Muhuri wa Saba,  
Ili aone mwenendo wa Ibilisi.

### 136. B) MICAIAH A TRUE WITNESS

1. There was peace in Israel,  
After 2 wars with Syria,  
Here we stand this day,  
Between the 2nd and 3rd woe.

**One like Micaiah is here,  
Holding to Elijah's Message,  
I am one like Micaiah,  
A true witness of Christ.**

2. There was a prophet in the land,  
Whose eyes were opened,  
To see the prophecy of the day,  
Micaiah a type of the Bride.
3. Ahab's agent tried to woo Micaiah,  
But Micaiah's confession was,  
I'll say what Jehovah tells me,  
He was Jehovah's true witness.
4. The Bride will do God's will,  
None will make her do otherwise  
She has thus says The Lord,  
Or She will just keep still.
5. Micaiah saw a lying spirit,  
Get into Ahab's prophets,  
Like 3 frogs in Revelation 16,  
To lead kings to Armageddon.
6. The Spirit of Elijah is here,  
To anoint the Bride today,  
Revealing the 7th Seal to her,  
And She sees the devil's move.

### 137. A) KUFA NA KUFUFUKA KWA LAZARO VYAFUNUA UKOMBOZI

1. Yesu akawa mbali Lazaro alipougua,  
Mariamu na Martha wakamtumania,  
Lazaro akafa kabla Yesu kurejea,  
Alipofika akasema Ye ni uzima na ufufuo.



**Tumeutwaa uzima na ufufuo,  
Sawa na alivyo Bwana Yesu,  
Tubadilishwe miili sote tunyakuliwe,  
Twende karamuni ya Mwanakondoo**

2. Lazaro alikuwa kaburini siku nne,  
Mfano wa watakatifu wa nyakati saba,  
Walio chini ya upako aina nne,  
Hata wengine kizazini chetu waliolala.
3. Yesu akawaagiza watoe jiwe kaburini,  
Akamwita Lazaro naye akafufuka,  
Bi-Arusi anayo huduma hiyo pia,  
Ya kuwaita watakatifu wale waliolala.
4. Mariamu, Martha, Lazaro naye Yesu,  
Wakaketi chakulani pamoja baadaye,  
Mfano wa karamu ya Mwanakondoo mbinguni,  
Ikiwa ni waliofufuka, nasi na Yesu.
5. Muhuri wa saba umefunuliwa,  
Tunao uzima wake tuite wengine,  
Wale wote walio wa tabaka letu,  
Tudhihirishwe tu wana wa Mungu kweli

### **137. B) LAZARUS DEATH AND RESURRECTION REVEAL REDEMPTION**

1. Jesus had left when Lazarus fell sick,  
Mary and Martha sent for Him,  
Lazarus died before Jesus arrived,  
He came and said, "I am the life and resurrection."

**We have possessed life and resurrection,  
Just like our Lord Jesus Christ,  
Our bodies will be changed for the Rapture,  
We will go to the marriage Supper in Heaven.**

2. Lazarus had been in the grave four days,  
A type of the Saints of the 7 church ages,  
Who are under the 4 anointing,  
Even some have slept in our age.
3. Jesus told them to take away the stone,  
He called and Lazarus came forth,  
The Bride of Christ has the same ministry,  
To wake up the saints who slept in the ages.
4. Mary, Martha, Lazarus and Jesus,  
Afterwards sat together for the evening meals,  
A type of the marriage Supper in Heaven,  
Of the resurrected, the living and Jesus.

5. The seventh seal has been revealed,  
We have the life to call the others,  
All those belong to the Bride of Jesus,  
To manifest that we are truly God's sons.

### **138. A) USIOGOPE BI-ARUSI MDOGO**

1. Hao pepo milioni mia mbili,  
Ndani ya baraza la makanisa,  
Wanajiandaa kusudi watutese,  
Kama tu na kanisa la kwanza.
- Usiogope Bi-arusi mdogo,  
Ni mapenzi ya Baba yetu,  
Kutupatia ufalme Wake,  
Tu wateule kwa neema Yake.**
2. Watatutawanya kama Yuda,  
Na kutudhulumu kama Danieli,  
Bali huo moto wao utazimwa,  
Na vinywa vya simba kufungwa.
  3. Japo tutatawanyika,  
Tungali wamoja kwa Roho,  
Na japo tuyapate mateso,  
Sisi tu zaidi ya washindi.

4. Tutajaza kikombe cha mateso,  
Na kuwa washindi kama Kristo,  
Twaemwa na mfumo wa dunia,  
Twaenda karamuni mbinguni.
5. Huo Mwaliko watukusanya,  
Watufanya wamoja kwa Roho,  
Mchuano wa Mlima Zayuni waja,  
Baragumuni ya mwisho tutapaa.
6. Ni saa ya Upendo mkamilifu,  
Twaondolewa uoga wote,  
Ni saa ya hiyo imani kamilifu,  
Kuweza kudhibiti hali aina zote.

### **138. B) FEAR NOT LITTLE BRIDE**

1. The 200 million devils  
In the world council of churches,  
Are set to persecute us,  
Just like in the Alpha church.

**Fear not little Bride,  
It's the Father's good will,  
To give us the Kingdom,  
You're elected by His grace.**



2. They'll scatter us like Judah,  
And persecute us like Daniel,  
But the fire will be quenched,  
And the lions' mouths shut.
3. Though we'll be scattered,  
We're still one in the Spirit,  
Though we be persecuted,  
We're more than conquerors.
4. We'll fill His cup of suffering,  
And overcome like Christ,  
Squeezed out of this system,  
For the marriage feast on high.
5. The Shout is gathering us,  
Uniting us by one Spirit,  
For Mt. Zion showdown,  
In the last trump we'll go home.
6. It's time for perfect Love,  
To cast out all fear,  
It's time for perfect faith,  
To master all circumstances!

### **139. A) BI-ARUSI AFANYIKA UNABII WAKE**

1. Elohim alirudi kwake Sarah,  
Hapo miili yao ilipobadilishwa,  
Isaka mwana wa ahadi akazaliwa,  
Mwanzo 18 ikafanyika historia.  
  
**Leo Maandiko haya yanatimia,  
Neno li ndani ya Bi-arusi wa Omega,  
Afunikwa na Nguvu za kuhuisha,  
Na kufanyika sauti ya mwisho leo**
2. Yesu alipoumbika ndani ya Mariamu,  
Isaya 7 ikawa historia kwake,  
Neno sasa li ndani ya Bi-arusi,  
Naye anayo Hivi asema Bwana.
3. Siku ya Pentekoste ilipotimia,  
Roho aliyeahidiwa akashuka,  
Juu yao waliomwamini Yesu,  
Yoeli 2 nayo ikawa historia kwao.
4. Yule Malaika Mkuu alishuka,  
Kwake nabii jangwani Arizona,  
Mihuri yote Saba ikafunuliwa,  
Ufunuo 10:1-7 ni historia sasa.

5. Nasi tutapitia njia hii tena,  
Akasema Roho katika nabii,  
Nayo Ufunuo 10:8-11,  
Inafanyika historia ndani yangu.

#### **Daraja**

**Roho wa Bwana Yu juu yangu,  
Neno lafanyika mwili ndani yangu,  
Mi waraka wa kusomwa na wote,  
Unabii kunihusu unakua historia**

### **139. B) THE BRIDE BECOMING HER OWN PROPHECY**

1. Elohim returned to visit Sarah,  
When their bodies were changed,  
Isaac the promised son was born,  
Then Genesis 18 became history.

**This day this Scripture is fulfilled,  
The Word is now in the Omega Bride,  
Overshadowed by the quickening power,  
Makes her the final voice today.**

2. When Jesus was forming in Mary,  
Isaiah 7 became history in her,  
The Word is now in the Bride,  
She has Thus Saith The Lord.
3. When the day of Pentecost came,  
The promised Holy Ghost descended,  
And Joel 2 became history in them,  
Upon those who believed Jesus.
4. The Mighty Angel descended,  
To the prophet in Arizona desert,  
Them seven seals were opened,  
Revelation 10:1-7 is history.
5. We will ride this trail again,  
Said the Spirit in the prophet,  
Revelation 10:8-11,  
Is now becoming history in me.

#### **Bridge**

**The Spirit of the Lord is upon me,  
His Word is becoming flesh in me,  
I'm now a living epistle read of all men,  
Prophecy is now becoming history in me!**

